*Mfululizo wa Masuala ya Kifikihi*

*al-Jam' Baina 's-Salaatayn*

# KUKUSANYA SALA MBILI

**Kwa Mtazamo wa Qur'ani na Sunna**

Kimeandikwa na:
**Sheikh Jafar Subhani**

Kimetarjumiwa na:
**Hemedi Lubumba Selemani**

**Haki ya kunakili imehifadhiwa na:**
**AL-ITRAH FOUNDATION**

**ISBN: 978 - 9987 - 427 - 41 - 3**

Kimeandikwa na:
**Sheikh Jafar Subhani**

Kimetafsiriwa na:
**Hemedi Lubumba Selemani**

Kimehaririwa na:
**Ustadh Abdallah Mohamed**

Toleo la kwanza: Julai 2007
Nakala 1000
Toleo la Pili: Machi, 2014
Nakala 1000

Kimetolewa na kuchapishwa na:
**Al -Itrah Foundation**
S. L. P - 19701, Dar-es-Salaam, Tanzania
Simu: +255 22 2110640 / 2127555
Barua pepe: alitrah@raha.com
Tovuti: www.ibn-tv.com
Katika mtandao: www.alitrah.info

# YALIYOMO

Kukusanya sala mbili.......................................................2
Kukusanya sala mbili Muzdalifa na Arafa......................3
Kukusanya kati ya sala mbili safarini......................... .....5
Kukusanya sala mbili bila udhuru pasipo safari.............19
Mgawanyo wa nyakati ndani ya Fiqhi ya Kisuni..........26
Anayeafikiana na Imamiyya katika baadhi ya mambo...27
Sunni wanaoafikiana na Imamiyya katika hili................29
Kukusanya bila udhuru kwa mujibu wa Sunna.............35
Wanazuoni wengi wameacha kuifanyia kazi.................50
Hadithi haielezi kukusanya kwa kutanguliza au kwa kucheleweshа.............................................................. 55
Alikusanya sala mbili kimuonekano............................ 58
Dalili za As-Shaukaniy za kuthibitisha kuwa kukusanya

kulikuwa kwa kimuonekano ..........................................62
Alikusanya kwa sababu ya udhuru usiyo julikana ........74
Maswali na majibu.........................................................79
(a) Ya kwanza: Mgongano wa Hadithi ya kuku
sanya na ile ya hanashu..............................79
(b) Ya pili: Mgongano wa Hadithi ya kukusanya
na ile ya usiku wa harusi............................81
(c) Ya tatu: Hadithi ya Habib bin Thabit si
hoja...........................................................83

# Neno la mchapishaji

Kitabu kilichoko mikononi mwako, ni tarjuma ya kitabu cha Kiarabu kwa jina la: "**Al-Jam'u Bayna Salaatayn**" Sisi tumekiita: "**Kukusanya Sala mbili.**"

Kitabu hiki, "Kusanya Sala mbili" ni matokea ya utafiti wa kielimu uliofanywa na Mwanachuoni wa Kiislamu, **Sheikh Jafar Subhani.**

Sheria ya Kiislamu ni ya kipekee kwa kuwa inahusika na kila jambo huku ikiweka utatuzi wa matatizo yote yanayompata mwanadamu katika sekta zote za maisha yake.

Wanachouni wa Kiislamu kama kawaida ya wanadamu wamehitilafiana katika hukumu ndogo ndogo katika matendo ya ibada, lakini kama ilivyo, tofauti ndogo kati ya wanachuo kwa wafuasi inakuwa ni mlima wa tofauti na kusababisha zongo lisilo na maana. Mambo ambayo wanachuo wetu wamehitilafiana si katika asili au misingi ya dini, na isitoshe ni mambo machache sana ukilingan-

isha na yale tunayokubaliana nayo.
Kukusanya Sala mbili ni suala ambalo wanachuo wetu wamehitalifiana; ndani ya madhehebu moja na kati ya madhehebu. Kwa hiyo hii sio hitilafu ya madhehebu, bali ni hitilafi ya wanachuo wa madhehebu zote wamehitilafiana juu ya suala hili. Lakini bahati mbaya Waislamu wengi hawaitambui hitilafu hii kwa usahihi na hivyo kuongelea katika dhana na kusababisha mizozo isiyokuwa na maana. Kutokana na hali hii Sheikh wetu, Jafar Subhani amelifanyia utafiti wa kina suala hili na kuweka wazi asaili ya hitilafu hii, kisha akamuachia msomaji mwenyewe kutoa uamuzi.

Kitabu hiki ni chenye manufaa sana, hususan wakati huu wa maendeleo makubwa ya elimu katika nyanja zote. Kutokana na ukweli huu, Taasisi yetu ya 'Al-Itrah Foundation' imeona ikitoe kitabu hiki kwa lugha ya Kiswahili, kwa madhumuni yake yale yale ya kuwahudumia Waislamu, hususan wazungumzaji wa Kiswahili, ili kuongeza ujuzi wao katika masuala ya dini na ya kijamii.

Tunamshukuru ndugu yetu, Hemedi Lubumba Selemani kwa kukubali jukumu hili la kukifanyia tarjuma kitabu hiki. Vilevile tunawashukuru wale wote walioshiriki kwa

njia moja au nyingine hadi kufanikisha kuchapishwa kwa kitabu hiki.

**Mchapishaji:**
**Al-Itrah Foundation**

# KUKUSANYA SALA MBILI

## Kwa Mtazamo wa Qur'ani na Sunna

Kila sifa njema ni za Mwenyezi Mungu, Mola wa ulimwengu. Rehma na Amani zimfikie mbora wa viumbe na hitimisho la mitume Wake, pia kizazi chake kitakatifu ambacho ndio kasha la elimu yake na hazina ya mafunzo yake.

Hakika Uislamu ni imani na sheria. Imani ni kuamini Mwenyezi Mungu, mitume Wake na Siku ya Mwisho.
Na sheria ni hukumu za Mwenyezi Mungu ambazo zina jukumu la kumpa mwanadamu maIsha bora na kumhakikishia wema wa dunia na akhera.

Sheria ya Kiislamu ni ya kipekee kwa kuwa inahusika na kila jambo huku ikiweka utatuzi wa matatizo yote yanayompata mwanadamu katika sekta zote za maIsha yake, hivyo Mwenyezi Mungu akasema:

﴿ ٱلۡيَوۡمَ أَكۡمَلۡتُ لَكُمۡ دِينَكُمۡ وَأَتۡمَمۡتُ عَلَيۡكُمۡ نِعۡمَتِي وَرَضِيتُ
لَكُمُ ٱلۡإِسۡلَٰمَ دِينٗاۚ ٣ ﴾

**“Leo nimewakamilishieni dini yenu na kuwatimizieni neema Yangu na nimewapendeleeni Uislamu uwe dini yenu.” (5:3).**

Isipokuwa kuna masuala madogo madogo ambayo wanazuoni wa sheria wametofautiana kwa sababu ya kuhitilafiana kwao kuhusu riwaya zitokanazo kwa Mtume (s.a.w.w.). Jambo ambalo limepelekea kutofautiana kuhusu masuala madogo madogo ya sheria.

Kwa kuwa ukweli hutokana na utafiti, basi hakika katika mtiririko wa masomo haya tumejaribu kuliweka suala hili juu ya meza ya utafiti, kwani huenda ikawa ndio njia ya kuunganIsha mtazamo na kusogeza hatua katika uwanja huu, kwani tofauti iliyopo si katika asili na misingi ya dini hata ipelekee kuwa na uadui na chuki, bali tofauti iliyopo ni kuhusu riwaya zilizonasibishwa na Mtume, nalo ni jambo dogo ukilinganIsha na mambo mengi ambayo tunaafikiana kati ya madhehebu za Kiislamu.

Na muongozo wetu katika njia hii ni kauli ya Mwenyezi Mungu (s.w.t):

﴿ وَٱعْتَصِمُوا۟ بِحَبْلِ ٱللَّهِ جَمِيعًا وَلَا تَفَرَّقُوا۟ ۚ
وَٱذْكُرُوا۟ نِعْمَتَ ٱللَّهِ عَلَيْكُمْ إِذْ كُنتُمْ أَعْدَآءً فَأَلَّفَ
بَيْنَ قُلُوبِكُمْ فَأَصْبَحْتُم بِنِعْمَتِهِۦٓ إِخْوَٰنًا ﴿١٠٣﴾ ﴾

**“Na shikamaneni na kamba ya Mwenyezi Mungu nyote wala msifarikiane. Na kumbukeni neema ya Mwenyezi Mungu iliyo juu yenu, mlipokuwa maadui na akaziunganIsha nyoyo zenu, hivyo kwa neema zake mkawa ndugu." (3:103).**

**Ja’far Subhani**
**Taasisi ya Imam Sadiq (a.s.)**
**Qum**

بسم الله الرحمن الرحيم

# KUKUSANYA SALA MBILI

Kukusanya kati ya Sala mbili kuna sura tofauti:

Kukusanya Sala mbili Muzdalifa na Arafa.

Kukusanya Sala mbili safarini.

Kukusanya Sala mbili pasipokuwa safarini kwa udhuru kama vile mvua na tope.

Kukusanya Sala mbili pasipokuwa safarini bila ya kuwepo udhuru wowote.

Hivyo sura mbili za kwanza ndizo zinazoingia katika hukumu ya safari na si sura mbili za mwisho. Wanazuoni wa sheria ya Kiislamu wamekubaliana kuhusu kukusanya Sala hapo Muzdalifa na Arafa lakini wametofautiana kuhusu kukusanya Sala eneo lingine lisilokuwa kati ya hayo mawili. Hivyo sisi hapa tutazungumzia kwa ufupi sura moja baada ya nyingine huku tukitaja kauli zinazohusu suala hili na vyanzo vya kauli hizo.

## 1. Kukusanya Sala mbili Muzdalifa na Arafa

Wanazuoni wa sheria ya Kiislamu wamekubaliana kuhusu kupendelea kukusanya Sala Muzdalifa na Arafa na wala hakuna tofauti katika hilo.

Al-Qurtuby amesema: "Wamekubaliana kuwa ni sunna kukusanya kati ya Adhuhuri na Al-Asr wakati wa Adhuhuri uwapo Arafa, na kati ya Magharibi na Isha wakati wa Isha uwapo Muzdalifa, huku wakitofautiana kuhusu kukusanya sehemu nyingine zisizo hizo mbili. [1]

Ibnu Quddama amesema: "Al-Hasan na Ibnu Sirin na watu wa rai wote wamesema: "Hairuhusiwi kukusanya isipokuwa siku ya Arafa uwapo Arafa, na usiku wa Muzdalifa uwapo Muzdalifa."[2]

Amepokea Muslim toka kwa Jabir bin Abdillah kuwa Mtume wa Mwenyezi Mungu alikaa miaka tisa bila kuhiji, kisha akawatangazia watu mwaka wa kumi kuwa

[1] *Bidayatul-Mujtahid* Juz. 1 / Uk. 170 chini ya anuani: sehemu ya pili kuhusu kukusanya Sala.

[2] *Al-Mughny:* Juz. 2, Uk. 112.

Mtume (s.a.w.w.) atahiji, hivyo watu wengi wakaenda Madina huku wote wakitaka waongozwe na Mtume na wafanye kama atakavyofanya. - Akaendelea mpaka akasema - mpaka alipofika Arafa akakuta quba limepambwa kwa madoa, akashuka hapo mpaka jua lilipopinduka, akaamrIsha aletewe ngamia, akaondoka mpaka alipofika ndani ya bonde akatoa hotuba - akaendelea mpaka akasema - kisha akaadhini na akakimu, akaswali Sala ya Adhuhuri, kisha akakimu akaswali Sala ya Al-Asr wala hakuswali chochote baina ya hizo mbili, - akaendelea mpaka akasema - akaenda mpaka akafika Muzdalifa, hapo akaswali Sala ya Magharibi na Isha kwa adhana moja na iqama mbili wala hakufanya tasbihi yoyote baina ya Sala hizo mbili. [3]

Kwa kuwa suala hili ni jambo linalokubalika kwa Waislamu wote basi tutafupIsha kwa kiasi hiki.

[3] *Sahih Muslim*: Juz. 4, uk. 39 - 42 mlango: Hija ya Mtume.

## Kukusanya kati ya Sala mbili safarini

Wanazuoni wengi wa Kiislamu wamekubaliana kuhusu kukusanya Sala mbili safarini isipokuwa Al-Hasan, An-Nakhai, Abu Hanifa na jamaa zake wawili. Hivyo inaruhusiwa kukusanya kati ya Adhuhuri na Al-Asr kwa kutanguliza kwa kuziswali wakati wa Sala ya mwanzo, na kwa kuchelewesha kwa kuziswali wakati wa Sala ya pili, hii ni kwa wote isipokuwa kwa hao tu.

Na Magharibi na Isha wakati mmoja kwa kuzitanguliza na kuzichelewesha.

Sala zinazokusanywa ni: Adhuhuri na Al-Asr, Magharibi na Isha katika wakati wa mojawapo ya hizo, huitwa kukusanywa hizo Sala za mwanzo *Jam'u taqdiim*, (kwa kutanguliza), na katika nyakati za Sala za pili huitwa *Jam'u taakhiri* (kukusanya kwa kuchelewesha).

As-Shaukani ametaja kauli mbali mbali kuhusiana na suala hili kwa namna ifuatayo:
Wanazuoni wengi wa sheria wameruhusu kukusanya

safarini kwa hali yoyote kwa kutanguliza na kuchelewesha, na kauli hii ndio ya maswahaba wengi na wanafunzi wa maswahaba na wanazuoni wa sheria huku miongoni mwao ni: At-Thaury, As-Shafy, Ahmad, Is'haqa na As-Shahaby.

Wengine wakasema: "Hairuhusiwi kukusanya kwa hali yoyote ile isipokuwa Arafa na Muzdalifa. Na hii ndiyo kauli ya Al-Hasan, An-Nakhai, Abu Hanifa na wenzake wawili.

Al-Laythu amesema: "Na kauli hii ni mashuhuri toka kwa Malik kuwa kukusanya kunamuhusu yule tu mwenye haraka na safari."

Ibnu Habibu amesema: "Kunamhusu mwenye kutembea."

Al-Awzay amesema: "Hakika kukusanya safarini kunamhusu mwenye udhuru."

Ahmad amesema: Inaruhusiwa kukusanya kwa kuchelewesha (*taakhiri*) na wala si kwa kutanguliza (*taqdiim*). Kauli hii ndio chaguo la Ibnu Hazm nayo ime-

pokewa toka kwa Malik.

Hizi ndizo kauli sita: Hivyo ikiwa suala kwa ufupi wamekubaliana wote isipokuwa wachache kama ulivyowaona, basi ni lazima tujadili suala hili sehemu mbili:

Je? Kukusanya kunamhusu tu yule mwenye haraka na safari.

Je? Inaruhusiwa kukusanya kwa kuchelewesha tu wala hakujumuishi kukusanya kwa kutanguliza?

Ama sehemu ya kwanza tunasema, habari zinazoonyesha kitendo cha Mtume (s.a.w.w) ziko katika makundi mawili: Kundi moja linaweka wazi kuwa alikuwa akikusanya awapo na haraka na safari, au aharakishwapo na safari:

Ameandika Muslim toka kwa Nafiu toka kwa Ibnu Umar kuwa Mtume wa Mwenyezi Mungu alikuwa akikusanya kati ya Magharibi na Isha awapo na haraka na safari.[4]

---

4 *Sahih Muslim,* Juz. 2, uk. 150 Kitabu cha Sala. Mlango: Ruhusa ya kukusanya Sala mbili safarini. Mlango wa Sala.

Ametoa Muslim toka kwa Salim, toka kwa baba yake: “Nilimuona Mtume wa Mwenyezi Mungu akikusanya kati ya Magharibi na Isha awapo na haraka na safari."

Ametoa Muslim toka kwa Salim bin Abdallah kuwa baba yake alisema: “Nilimuona Mtume wa Mwenyezi Mungu anapokuwa na haraka ya safari, akichelewesha Sala ya Magharibi mpaka anapokuja kuikusanya na Sala ya Isha.” **5**

Ametoa Muslim toka kwa Anas toka kwa Mtume kuwa aharakishwapo na safari huchelewesha Adhuhuri mpaka mwanzo mwa wakati wa Al-Asr hivyo huzikusanya pamoja, na huchelewesha Magharibi mpaka anapokuja kuikusanya na Isha pindi mawingu mekundu yanapozama.[6]

Kundi la pili linaonyesha kitendo cha Mtume wa Mwenyezi Mungu bila sharti lolote (iwapo ana haraka na safari).

---

[5] *Sahih Muslim*, Juz. 2, uk. 150 Kitabu cha Sala. Mlango: Ruhusa ya kukusanya Sala mbili safarini. Mlango wa Sala.

[6] *Sahih Muslim* Juz. 2 Uk. 151 Kitabu cha Sala. Mlango: Ruhusa ya kukusanya Sala mbili safarini. Mlango wa Sala

Ametoa Muslim toka kwa Anas bin Malik amesema: "Iwapo Mtume akianza safari kabla ya kupinduka jua alikuwa akichelewesha Adhuhuri mpaka wakati wa Al-Asr, kisha hushuka na kuzikusanya pamoja. Na iwapo jua litapinduka kabla ya safari, basi huswali Adhuhuri kisha hupanda kipando. [7]

Ametoa Muslim toka kwa Anas amesema: "Ilikuwa Mtume akitaka kukusanya kati ya Sala mbili safarini basi huchelewesha Adhuhuri mpaka mwanzoni mwa wakati wa Al-Asr kisha huzikusanya pamoja. [8]

Abu Daud na Tirmidhy wamepokea toka kwa Maadh bin Jabal kuwa: "Mtume alikuwa katika vita vya Tabuk anapotaka kusafiri kabla ya kupinduka kwa jua akachelewesha Adhuhuri mpaka akaja kuikusanya na Al-Asr pamoja, na anapotaka kusafiri baada ya kupinduka jua, huswali Adhuhuri na Al-Asr pamoja kisha huondoka, na ilikuwa akitaka kuondoka kabla ya Magharibi,

---

7 *Sahih Muslim*, Juz. 2, Uk. 151 Kitabu cha Sala. Mlango: Ruhusa ya kukusanya Sala mbili safarini. Mlango wa Sala

8 *Sahih Muslim,* Juz. 2 Uk. 151 Kitabu cha Sala. Mlango: Ruhusa ya kukusanya Sala mbili safarini. Mlango wa Sala

huichelewesha Magharibi mpaka aiswali na Isha pamoja, na ilikuwa akitaka kuondoka baada ya Magharibi huitanguliza Isha na kuiswali na Magharibi pamoja. [9]

Ahmad amepokea ndani ya *Musnad* yake toka kwa Abbas` (r.a.) toka kwa Mtume kuwa Mtume akiwa na safari alikuwa kabla ya kupanda kipando hukusanya Sala za Adhuhuri na Al-Asr iwapo jua limepinduka akiwa nyumbani kwake.

Na iwapo halijapinduka akiwa nyumbani kwake, basi huondoka mpaka unapofika wakati wa Al-Asr ndipo hushuka kisha hukusanya Adhuhuri na Al-Asr. Na iwapo Magharibi itaingia akiwa nyumbani kwake basi hukusanya Magharibi na Isha pamoja, na iwapo Magharibi haijaingia akiwa nyumbani kwake huondoka mpaka Isha inapoingia ndipo hushuka na kuzikusanya pamoja.[10]

---

9 *Sunan Abi Daud*: Juz. 2, uk. 8 Kitabu cha Sala mlango: Kukusanya Sala mbili. Hadithi ya 1220

10 *Musnad Ahmad bin Hambal:* Juz 5 Uk. 241, *Sunan Abi Daud*: Juz. 2, uk. 2 kitabu cha Sala mlango: Kukusanya kati ya Hadithi mbili 1220

Baada ya As-Shaukany kunukuu riwaya hii akasema: Shafy amepokea riwaya hii katika *Musnad* yake kwa namna yake akasema: "Na akiondoka kabla jua halijapinduka hucheleweshá Adhuhuri mpaka aje aikusanye na Al-Asr wakati wa Al-Asr."[11]

Nasema: Kanuni ni kuchukuwa chenye sharti maalumu na kukitanguliza kabla ya kisicho na sharti maalumu, hivyo kuziwekea riwaya zisizo na sharti maalum lile sharti maalum lililomo kwenye riwaya zenye sharti maalumu, ndio maana hata Anas kanukuu kitendo cha Mtume bila ya kuwa na sharti maalumu na mara nyingine kikiwa na sharti maalumu. [12]

Naongeza kuwa riwaya zinazoonyesha kitendo cha Mtume ni dalili ya ufahamu si tamko la Mtume, na suala linapokuwa hivi linakuwa halina sifa ya kuwa au kutokuwa sharti, kwa sababu hali hii ya kuwa au kutokuwa sharti ni hali ya tamko si ya kitendo, na wala

---

11 *Naylul-Awtwar:* Juz. 3, Uk. 213

12 *Bidayatul-Mujtahid:* Juz. 1, Uk. 173 Chapa nyingine iliyohakikiwa: Juz. 2, Uk. 374.

katika suala hili hakuna tamko lolote lililopokewa toka kwa Mtume bali ni kitendo alichokinukuu mpokezi, na huenda kitendo chake hiki kilikuwa kimekutana na hali ya kuwa na haraka na safari, na ikawa mpokezi hakutaja hali hii kwa kutegemea kuwa haihusiki na hukumu.

Kutokana na haya maelezo hakusanyi isipokuwa anapokuwa na haraka na safari. Na inawezekana ndilo alililoliashiria Ibnu Rushdi aliposema: "Kukusanya kumenukuliwa kwa kitendo tu." [13]

Na kinachoweza kuipa nguvu kauli ya pili (bila sharti maalum) ni kuwa sharti lililopo katika riwaya hizi (iwapo ana haraka na safari) ni miongoni mwa masharti yatokanayo na hali ya mara kwa mara, masharti ambayo huwa hayafahamiki kama sharti, hiyo ni mfano wa kauli ya Mwenyezi Mungu: **"Na binti zenu wa kambo walio katika ulinzi wenu, waliozaliwa na wake zenu mliowaingilia"**[14] Hakika binti wa kambo ameharamish-

[13] *Bidayatul-Mujtahid*: Juz. 1, Uk. 173 Chapa nyingine iliyohakikiwa: Juz.2 Uk. 374

[14] Nisaa; 4: 23

wa, sawa awe katika ulinzi wa mwanaume au hapana, lakini mara nyingi mwanamke anapoolewa huenda na binti yake kwa mume wa pili. Kwa ajili hiyo binti yeyote wa kambo ni haramu bila sharti lolote sawa awe katika ulinzi wa mwanaume au hapana.

## Kukusanya Sala mbili pasipo na safari kwa ajili ya udhuru

Jambo lililo mashuhuri ni kuwa inaruhusiwa kukusanya kati ya Magharibi na Isha kwa ajili ya udhuru kinyume na Hanafiyya ambao hawajaruhusu kukusanya kwa hali yoyote ile isipokuwa msimu wa Hijja uwapo Arafa au Muzdalifa.

Ama wanaoruhusu kukusanya nao wametofautiana kwa namna zifuatazo:

Je ruhusa inahusu mvua tu au inajumuisha udhuru mwingine?

Je ruhusa inahusu Magharibi na Isha au inajumuisha Adhuhuri na Al-Asr?

Je ruhusa inahusu kukusanya kwa kutanguliza tu au inajumuisha kukusanya kwa kuchelewesha?[15]

Yafuatayo ni maneno yao kuhusu sura hizo tatu:
Ya kwanza: Dhahiri toka kwa Shafy ni kuwa ruhusa inahusu mvua tu.

As-Shiraziy amesema: "Inaruhusiwa kukusanya Sala mbili katika hali ya mvua. Hairuhusiwi kukusanya kwa ajili ya hali ya upepo mkali, tope, ugonjwa na giza."[16]

(1). Ibnu Rushdi amesema: "Shafi ameruhusu kukusanya usipokuwa safarini kwa ajili ya mvua, - mpaka aliposema - ama kukusanya kwa ajili ya ugonjwa usipokuwa safarini ni kuwa Malik ameruhusu iwapo atahofia kuzimia au ana ugonjwa wa tumbo, lakini Shafy kakataza hilo.[17]

(2). Akasema ndani ya kitabu *As-Sharhul-Kabiru* kuwa: Na je ni ruhusa hilo - kinyume na mvua - kwa ajili ya tope

15 Tuliyoyataja ni vichwa vya tofauti zao, lakini matawi yake ni mengi hatuna haja ya kuyaingilia

16 *Al-Majmuu*: Juz. 4, Uk. 258, Kifungu cha matni

17 *Bidayatul-Mujtahid*: Juz. 1, Uk. 173-174 mahali pawili

na upepo mkali wenye baridi, au kwa mwenye kuswalia nyumbani au msikitini huku njiani kuna mvua nyingi.[18]

Ya pili: Yaani je ruhusa inahusu Magharibi na Isha tu au inajumuisha Adhuhuri na Al-Asr? Ibnu Rushdi amesema: "Shafy ameruhusu kukusanya usipokuwa safarini kwa udhuru wa mvua usiku au mchana, ama Malik yeye ameruhusu usiku akakataza mchana.[19]

An-Nawawy amesema: "Shafy na jamaa wamesema inaruhusiwa kukusanya Adhuhuri na Al-Asr, Magharibi na Isha katika hali ya mvua. Imam wa haramaini akaeleza kuwa inaruhusiwa kukusanya Magharibi na Isha wakati wa Magharibi, wala hairuhusiwi kati ya Adhuhuri na Al-Asr, na haya ndio madhehebu ya Malik.

Al-Mazny amesema: "Hairuhusiwi kwa hali yoyote. Madhehebu ya kwanza ndiyo yanayotokana na maelezo ya Shafy, ya zamani hadi mapya."[20]

---

18 *Al-Mughni*, Juz. 2, Uk. 118

19 *Bidayatul-Mujtahid*, Juz. 1, Uk. 173

20 *Al-Majmuu*: Juz. 4, Uk. 260

Ya tatu: Yaani ruhusa inahusu kukusanya kwa kutanguliza bila kujumuisha kukusanya kwa kuchelewesha.

A-Shirazy amesema: "Ni ruhusa kukusanya Sala mbili katika hali ya mvua katika wakati wa Sala za kwanza, na je inaruhusiwa kuzikusanya katika wakati wa Sala za pili?" Hapa kuna kauli mbili: Shafy amesema ndani ya *Al-Imlau*: "Inaruhusiwa kwa sababu ni udhuru unaoruhusu kukusanya katika wakati wa Sala ya mwanzo hivyo ikaruhusiwa kukusanya katika wakati wa Sala ya pili kama kukusanya kwa safarini.

Akasema katika *Al-ummu*: "Hairuhusiwi kwa sababu iwapo akichelewesha huenda mvua ikakatika hivyo akawa kakusanya bila udhuru."[21]

Huu ni ufupi wa kauli katika nukta hizi tatu. Pia wao wana tofauti katika sehemu nyingine ambazo hakuna haja ya kuzitaja.

Baada ya kutambua hilo la muhimu ni kuwepo dalili juu ya ruhusa ya kukusanya kwa udhuru usipokuwa safarini.

21 *Al-Majmuu*: Juz, 4. Uk. 258

Wamethibitisha hilo kwa Hadithi mbili:
Inayoonyesha kuwa inaruhusiwa kukusanya usipokuwa safarini katika hali yoyote ile, hivyo wakaichukulia katika hali ya mvua au udhuru wowote ule. Bukhari ametoa toka kwa Ibnu Abbas` (r.a.) kuwa Mtume aliswali Madina rakaa saba na rakaa nane, yaana Adhuhuri na Al-Asr, Magharibi na Isha.[22] Ibnu Rushdi amesema: "Ama kuhusu kukusanya usipokuwa safarini bila udhuru wowote ni kuwa Malik na wanazuoni wengi hawaruhusu, lakini hilo limeruhusiwa na wengi kati ya kundi la dhahiri na Ash'habu ambaye ni kati ya wafuasi wa Malik. Sababu kubwa ya kutofautiana kwao ni tofauti yao kuhusu ufahamu wa Hadithi ya Ibnu Abbas`, hivyo wapo waliyoitafsiri kuwa ilikuwa ni katika hali ya mvua kama alivyosema Malik, na wapo walioichukulia kuwa ni hali yoyote.

Aliyoipokea Ibnu Abbas` kuwa Mtume alikusanya Adhuhuri na Al-Asr na kati ya Magharibi na Isha Madina bila ya hofu, safari wala mvua. Akaulizwa Ibnu Abbas: Alitaka nini katika hilo? Akasema: "Alitaka asiutaabishe

22 Katika sura ya nne utaona vyanzo vya riwaya hizi.

umma wake."[23]

Dhahiri inaonyesha kuwa kukusanya wakati wa hali ya mvua ni jambo lililokuwa linajulikana kabla, ndio maana Ibnu Abbas` alijaribu kubainisha kuwa kukusanya huku hakukuwa ni kwa lengo la mvua au nyudhuru nyingine bali ilikuwa ni msamaha kwa lengo la kutokuutaabisha umma wake. Hivyo ikiruhusiwa kukusanya katika hali isiyo ya safari kwa udhuru wowote, basi kukusanya safarini bila udhuru wowote itakuwa ni hiyari kati ya hukumu za safari. Kwa sababu msafiri atakusanya Sala mbili safarini bila udhuru.

Ama yule asiye safarini yeye atakusanya kwa ajili ya udhuru au kwa lengo lingine. Ama tukisema kuwa inaruhusiwa kukusanya bila udhuru wowote usipokuwa safarini, basi haitakuwa kukusanya kati ya Sala mbili ni kati ya hukumu za safari.

Mpaka hapa maneno yametimia kuhusu sura ya tatu, hivyo imebakia sura ya nne.

---

[23] Katika sura ya nne utaona vyanzo vya riwaya hizi.

# Kukusanya Sala mbili bila udhuru pasipo safari

Imamiyya wameafikiana kuwa inaruhusiwa kukusanya Sala mbili bila ya udhuru wowote pasipo safarini, japokuwa kutenganisha ni bora.

Sheikh Tusi amesema: "Inaruhusiwa kukusanya Sala mbili kati ya Adhuhuri na Al-Asr na kati ya Magharibi na Isha, uwapo safarini au usipokuwa safarini na katika hali yoyote ile. Wala hakuna tofauti kati ya kukusanya wakati wa Sala ya mwanzo au wakati wa Sala ya pili. Kwa sababu wakati wa baada ya kupinduka jua ni wakati wa kushirikiana, na wakati wa baada ya Magharibi ni wakati wa kushirikiana pia kama tulivyobainisha.[24]

Hakika upande wa madhehebu ya Imamiyya haina maana kuwa kukusanya Sala mbili ni kuiswali Sala nje ya wakati wake wa kisheria, bali muradi wake ni kuiswali katika muda usiyo wa ubora. Hivyo ufuatao ni ufafanuzi wa

[24] *Al-Khilafu*: Juz. 1 Uk. 588 mas'ala ya 351 Huko mbele utaona jinsi wakati ulivyobainishwa

madhehebu yenyewe:
Kutokana na maelezo toka kwa Maimamu wa Ahlul-Bayt Imamiyya wamesema kuwa jua likipinduka basi umeingia wakati wa Sala mbili, yaani wakati wa Adhuhuri na Al-Asr, isipokuwa Sala ya Adhuhuri huswaliwa kabla ya Al-Asr, hivyo wakati uliyopo kati ya kupinduka jua na kuzama kwake ni wakati wa kushirikiana kati ya Sala mbili hizo.

Isipokuwa muda wa kutosha rakaa nne kabla ya kuzama kwa jua ni muda mahususi kwa ajili ya Sala ya Adhuhuri, na muda wa kutosha rakaa nne mwishoni mwa wakati ni wakati mahususi kwa ajili ya Sala ya Al-Asr, na muda uliyopo kati ya nyakati hizo mbili ni wakati wa kushirikiana kati ya Sala mbili.

Hivyo akiswali Sala ya Adhuhuri na Al-Asr katika muda wowote kati ya kupinduka jua na kuzama kwake atakuwa kaswali Sala hizi ndani ya wakati wake, kwa sababu ni wakati wa kushirikiana kati ya Sala mbili hizo.

Isipokuwa muda wa kutosha kuswali rakaa nne toka mwanzo wa wakati ni mahususi kwa ajili ya Adhuhuri hivyo haisihi kuswali Al-Asr humo.

Na muda wa kutosha kuswali rakaa nne mwishoni mwa wakati ni mahususi kwa ajili ya Al-Asr hivyo haisihi kuswali Adhuhuri humo.

Hii ndio hali halisi ya madhehebu, kwa ajili hiyo mwenye kukusanya Sala mbili nje ya wakati mahususi ametekeleza faradhi ndani ya wakati wake, hivyo Sala yake inakuwa ni kutekeleza (ndani ya wakati) na wala si kulipa.

Hivyo ni kuwa kila Sala ukiachilia mbali wakati wake wa kusihi bado ina wakati wake wa ubora. Hivyo wakati wa ubora wa Sala ya Adhuhuri ni kuanzia kupinduka kwa jua mpaka kivuli cha kitu kilichosimama kufikia urefu wa kipimo cha kitu chenyewe, baada ya kile kivuli cha mwanzo cha kabla ya kupinduka jua kuwa kimeondoka au kimetoweka.

Na mashuhuri ni kuwa wakati wa ubora wa Al-Asr ni kuanzia pale kivuli kinapolingana na kipimo mpaka pale kinapokuwa mara mbili ya kipimo husika.

Kwa wakati wa Magharibi na Isha hujulikana kuwa likizama jua zimeingia nyakati mbili mpaka nusu ya usiku.

Wakati wa mwanzo ni mahususi kwa ajili ya Magharibi kwa muda wa kutimiza Sala nzima, na wakati wa mwisho ni mahususi kwa Isha kwa muda wa kutimiza Sala nzima, na wakati uliyopo kati ya muda huo ni wakati wa kushirikiana.

Hivyo kila Sala kati ya Sala mbili hizi ina wakati wa ubora. Wakati wa ubora wa Magharibi ni kuanzia kuzama kwa jua mpaka kuondoka kwa wekundu wa Magharibi, na wakati wa ubora wa Isha ni kuanzia kuondoka kwa wekundu wa Magharibi mpaka theluthi ya usiku.[25]

Mara nyingi anayewashangaa Imamiyya kukusanya kati ya Sala mbili hudhani kuwa mwenye kukusanya huswali moja ya Sala mbili nje ya wakati wake, lakini amesahau kuwa mwenye kuswali huwa ameiswali nje ya wakati wa ubora lakini huwa ameiswali ndani ya wakati wa kusihi, na wala si ajabu Sala kuwa na nyakati tatu.

**Ya kwanza:** Wakati mahususi ni ule wa kutosha rakaa nne mwanzoni mwa kuingia wakati, na wakati wa mwisho ni

[25] Angalia *Al-Ur'watul-Wuthqa*: Uk. 171. Kipengele cha nyakati za Sala

pale unapokaribia kwisha wakati. Au rakaa tatu baada tu ya kuzama jua na rakaa nne kabla kidogo ya nusu ya usiku.

**Ya pili:** Wakati wa ubora ambao tayari maelezo yake yameshatangulia kuhusu Adhuhuri na Al-Asr, Magharibi na Isha.

**Ya tatu:** Wakati wa kusihi ambao ni wakati wote uliyopo kati ya vipimo viwili isipokuwa ule tu uliyo mahususi kwa moja ya Sala mbili, hivyo wakati wa kusihi unajumuisha wakati wa ubora na ule wa baada ya ubora.

As-Swaduq amepokea kwa isnadi yake toka kwa Zararatu toka kwa Abu Jafar (a.s.) alisema: "Jua likipinduka umeingia wakati wa Sala mbili: Adhuhuri na Al-Asr. Na jua likizama umeingia wakati wa Sala mbili: Magharibi na Isha ya mwisho."[26]

Shekhe Tusi amepokea toka kwa Ubaydu bin Zararatu alisema: "Nilimuuliza Aba Abdillah kuhusu wakati wa

[26] *Al-Faqihi*: Juz. 1 Uk. 140. Pia inapatikana kwenye Hadithi ya 1 mlango wa 17

Adhuhuri na Al-Asr. Akajibu: “Jua likipinduka umeingia wakati wa Adhuhuri na Al-Asr isipokuwa hii inakuwa kabla ya hii, kisha wewe unakuwa katika wakati ambao ni wa sala zote mbili mpaka jua lizame.”[27]

Riwaya zenye maana hii ni nyingi lakini sisi tunaishia hapa. Hivyo ikiwa Sala zina nyakati tatu kama tulivyobainisha basi inatubainikia kuwa kukusanya si jambo baya isipokuwa kinachokupita ni wakati wa ubora wala si wakati asili wa Sala, kwa ajili hiyo imepokewa toka kwa Maimamu wa Ahlul-Bayt kuwa kutenganisha ni bora kuliko kukusanya, hivyo hapa tutataja baadhi ya riwaya zinazoruhusu kukusanya ili tupate baraka tu kwani suala hili kwenye fiqhi ya shia Imamiyya ni suala la wazi sana.

Amepokea As-Saduqu toka kwa Abdallah bin Sanani toka kwa Swadiq (a.s.) kuwa Mtume wa Mwenyezi Mungu alikusanya Adhuhuri na Al-Asr kwa adhana moja na iqama mbili, na akakusanya Magharibi na Isha kwa adhana moja na ikama mbili, bila ya kuwa safarini na bila ya udhuru wowote.[28]

27 *At-Tahadhibu*: Juz. 2, uk. 26

28 *Al-Faqihi*: Juz. 1, Uk. 186 namba 886

Pia amepokea toka kwa Is'haqa bin Ammar toka kwa Aba Abdillah alisema: “Hakika Mtume aliswali Adhuhuri na Al-Asr sehemu moja bila ya udhuru wala sababu yoyote. Umar akauliza: “Je kuna kitu kimezuka ndani ya Sala?” Akajibu: “Hapana isipokuwa nimetaka kuupa nafuu umma wangu.”[29]

Kulayny ametoa toka kwa Zararatu toka kwa Aba Abdillah amesema: “Mtume aliwaswalisha watu jamaa Adhuhuri na Al-Asr baada ya kupinduka jua bila ya udhuru wowote, na aliwaswalisha jamaa Magharibi na Isha kabla ya kuondoka wekundu wa Magharibi bila ya udhuru wowote, hakika alifanya hivyo ili aupe umma wake nafuu ya wakati.[30]

Na kuna riwaya nyingi ambazo amezikusanya shekhe Al-Hurru AlAamily ndani ya kitabu chake *Wasailul-Shia*. [31]

Mpaka hapa umebainika mtazamo wa Shia Imamiyya kuhusu kukusanya Sala mbili.

---

29 *Ilalul-Sharaiu*: 321 mlango wa 11

30 *Al-Kafiy*: Juz. 3 Uk. 286 Hadithi ya 1

31 *Al-Wasailu*: Juz.4 Uk. 220-223 mlango wa 32 kati ya milango ya nyakati.

# Mgawanyo wa nyakati ndani ya Fiqhi ya Kisunni

Huenda mtu asiyejua akadhani kuwa mgawanyo huu wa nyakati unahusu fiqhi ya Imamiyya tu, bali ni kuwa mgawanyo huu wa nyakati katika aina tatu unahusu fiqhi zote mbili japokuwa kunatofauti kuhusu muda wa wakati. Ndani ya *Sharhul-Muhadhabu* An-Nawawiy amesema: "**Tawi**: Adhuhuri ina nyakati tatu: Wakati wa ubora, wakati wa hiyari na wakati wa udhuru, hivyo wakati wa ubora ni mwanzoni mwa wakati, na wakati wa hiyari ni baada ya wakati wa ubora mpaka mwisho wa wakati, na wakati wa udhuru ni wakati wa Al-Asr kwa mwenye haki ya kukusanya kwa ajili ya safari au mvua."

Kisha akasema: Al-kadhi Huseini amesema: "Adhuhuri ina nyakati nne: Wakati wa ubora, wakati wa hiyari, wakati wa ruhusa, na wakati wa udhuru. Hivyo wakati wa ubora ni pale kivuli cha kitu kilichosimama kitakapofikia robo ya kipimo cha kitu hicho, na wakati wa hiyari ni kitakapofikia nusu yake, na wakati wa ruhusa ni kitakapolingana kivuli na hicho kitu na hapo ndio mwisho

wa wakati. Na udhuru ni wakati wa Al-Asr kwa mwenye kukusanya kwa ajili ya safari au mvua. [32]

## Anayeafikiana na Imamiyya katika baadhi ya nukta

Pia wapo wanaoafikiana na Imamiyya katika baadhi ya nukta za suala hili.

An-Nawawy amenukuu kwa kusema: Atwau na Tausi wamesema: "Kivuli cha kitu kikilingana na kitu chenyewe hapo umeingia wakati wa Al-Asr na ufuatao ni wakati wa Adhuhuri na Al-Asr kwa kushirikiana mpaka jua litakapozama.

Kauli hii inahusu Adhuhuri kwa kivuli cha kitu kulingana na kitu husika, kisha inafanya wakati uliobaki ni wa kushirikiana Adhuhuri na Al-Asr mpaka jua litakapozama. Kauli hii inakaribiana na ile ya Imamiyya.

32 *Al-Majmuu* Juz.3 Uk. 27

Malik amesema: "Kivuli kikilingana na kipimo cha kitu kilichosimama ndio mwisho wa wakati wa Adhuhuri na mwanzo wa wakati wa Al-Asr kwa kushirikiana. Hivyo kivuli kikizidi kipimo ziada ya wazi basi wakati wa Adhuhuri umekwisha.[33]

Kauli hii inafanya sehemu ya wakati kuwa wakati wa kushirikiana kati ya Adhuhuri na Al-Asr nao ni - baada ya kivuli kulingana na kipimo cha kitu kilichosimama - mpaka kivuli kinapokizidi kipimo hicho kwa ziada ya wazi, ni wakati wa kushirikiana kati ya Adhuhuri na Al-Asr.

Pia imenukuliwa toka kwake kuwa, wakati wa Adhuhuri unaendelea mpaka kuzama kwa jua.[34]

Na kuna kauli nyingine ambazo zina namna fulani ya muafaka na fiqhi ya Imamiyya.

---

33 *Al-Majmuu*, Juz. 3, Uk. 24

34 *Al-Majmuu*, Juz. 3, Uk. 27

## Masunni wanaoafikiana na Imamiyya katika kila kitu kuhusu suala hili

Japokuwa kukusanya Sala bila udhuru ni kati ya mambo ya wazi katika fiqhi ya Imamiyya lakini suala hili si mahususi kwa Imamiyya peke yao bali kuna baadhi ya wanazuoni wa sheria wa kisunni wameafikiana nao katika suala hili.

Ibnu Rushdi amesema: "Ama kukusanya bila udhuru usipokuwa safarini hakika Malik na wanazuoni wengi wa sheria hawaruhusu, lakini wameruhusu hilo baadhi ya jamaa katika watu wa Dhahir na Ash'habu katika wafuasi wa Malik. Na sababu ya kutofautiana kwao ni tofauti yao kuhusu kuifahamu hadith ya Ibnu Abbas, hivyo wapo walioifafanua kuwa ilikuwa kwa sababu ya safari, na wapo walioichukulia katika hali yoyote ile.

Muslim katika Hadithi yake ameondoa kauli: 'Bila ya hofu wala safari wala mvua.' Hili ndilo waliloshikilia watu wa Dhahir.[35]

---

[35] *Bidayatul-Mujtahid*, Juz. 2, Uk. 374 chapa iliyohakikiwa

An-Nawawy amesema: **Tawi**: "Kuhusu madhehebu yao kuna kukusanya bila hofu, safari, mvua, wala ugonjwa. Madhehebu yetu (ya Shafy) na madhehebu ya Abu Hanifa, Malik, Ahmad, na jamuhuri ni kuwa hairuhusiwi. Ibnu Al-Mundhir ameelezea kuhusu kundi linaloruhusu bila udhuru wowote. Akasema: Ibnu Sirin ameruhusu kwa ajili ya haja maalum au asipochukulia kama mazoea.[36]

Kwa namna yoyote ile la muhimu ni dalili si kauli, hivyo iwapo kauli zitaafikiana na dalili basi ni vizuri, na kama si hivyo basi marejeo ya mwisho ni dalili.

## Kukusanya Sala mbili kwa mujibu wa Kitabu (Qur'an)

Mwenyezi Mungu amesema: **"Simamisha Sala jua linapopinduka, mpaka giza la usiku na Qur'ani ya alfajiri. Hakika Qur'ani ya alfajiri inashuhudiwa"** [37]

Aya imebeba jukumu la kubainisha nyakati za Sala tano, hivyo iwapo tukisema makusudio ya giza la usiku ni nusu

36 *Al-Majumuu*, Juz. 4, Uk. 264
37 Israa; 17:78

ya usiku basi wakati uliyopo kati ya kupinduka kwa jua na giza la usiku utakuwa wa Sala nne, isipokuwa dalili imeonyesha kuwa wakati wa Adhuhuri na Al-Asr unakomea kwa kuzama jua, hivyo wakati uliopo kati ya kupinduka jua na kuzama jua ni wakati wa kushirikiana kati ya Adhuhuri na Al-Asr. Kama inavyokuwa wakati uliyopo kati ya kuzama kwa jua mpaka kuingia giza la usiku ni wakati wa kushirikiana kati ya Magharibi na Isha.
Na huenda mtu akafasiri giza la usiku kwa maana ya kuzama jua, hivyo Aya itakuwa imebeba jukumu la kubainisha wakati wa Adhuhuri, Al-Asr na Sala ya alfajiri bila kubainisha Magharibi na Isha. Na maarufu ni tafsiri ya mwanzo.

At-Tabarasiy amesema: "Katika Aya hii kuna dalili ionyeshayo kuwa wakati wa Sala ya Adhuhuri umerefushwa mpaka mwisho wa mchana, kwa sababu Mwenyezi Mungu alifanya wakati wa kuanzia kupinduka kwa jua ambako ndio kugeuka mpaka giza la usiku ni wakati wa Sala nne, isipokuwa Adhuhuri na Al-Asr zinashirikiana katika wakati mmoja nao ni kuanzia kugeuka kwa jua mpaka kuzama kwake.

Na Magharibi na Isha zinashirikiana katika wakati mmoja nao ni kuanzia kuzama kwa jua mpaka giza la usiku. Na Sala ya alfajiri ameitenganisha kwa kusema: 'Na Qur'ani ya alfajiri', hivyo Aya inabainisha wajibu wa Sala tano huku ikibainisha nyakati zake.[38]

Tuliyoyataja ndio maelezo aliyoyatoa Imam Al-Baqir (a.s.) aliposema: "Mwenyezi Mungu alimwambia Mtume wake: 'Simamisha Sala jua linapopinduka mpaka giza la usiku.' Hizi ni Sala nne alizozipa majina Mwenyezi Mungu, akazibainisha na kuziwekea nyakati. Na giza la usiku ni nusu ya usiku. Kisha Mwenyezi Mungu akasema: 'Na Qur'ani ya alfajiri, hakika Qur'ani ya alfajiri inashuhudiwa,' hii ni Sala ya tano."[39]

As-Sadiq (a.s.) amesema: "Ndani ya Aya hiyo kuna Sala mbili mwanzo wa wakati wake ni kupinduka kwa jua isipokuwa hii ni kabla ya hii. Na kuna Sala mbili mwanzo wa wakati wake ni kuzama kwa jua mpaka nusu ya usiku isipokuwa hii ni kabla ya hii."

---

38 *Maj'maul-Bayan*, Juz. 3, Uk. 434

39 *Nuru-Thaqalain*, Juz. 3, Uk. 202 Hadith ya 377

Al-Qurtuby amesema: "Kuna watu wameona kuwa wakati wa Sala ya Adhuhuri unaanzia kupinduka kwa jua mpaka kuzama kwake, kwa sababu Mwenyezi Mungu ameuweka wajibu wake kutegemeana na kupinduka kwa jua na wakati wote huu ni kupinduka kwa jua. Kauli hii kaisema kwa upana Al-Awzay na Abu Hanifa. Ama Malik na Shafy wenyewe wameashiria kauli hii wakati wa dharura.[40]

Ar-Raziy amesema: "Laiti tukitafsiri giza la usiku kwa maana ya kuingia kwa giza la mwanzo, basi ibara giza la usiku itamaanisha mwanzo wa Magharibi, kwa maana hii nyakati zilizotajwa na Aya zitakuwa tatu: Wakati wa kupinduka kwa jua, wakati wa kuanza Magharibi na wakati wa alfajiri."

Akasema: "Hili linapelekea kupinduka kwa jua kuwe ni wakati wa Adhuhuri na Al-Asr hivyo wakati huu unakuwa ni wa kushirikiana kati ya hizi Sala mbili.

Na mwanzo wa Magharibi uwe ni wakati wa Magharibi na Isha, hivyo uwe ni wakati wa kushirikiana kati ya hizi

40 *Al-Jamiu-liah'kamil-Qur'ani*, Juz. 1, Uk. 304

Sala mbili. Hii inapelekea kuruhusiwa kukusanya katika hali yoyote ile kati ya Adhuhuri na Al-Asr Magharibi na Isha, isipokuwa dalili inaonyesha kuwa kukusanya bila udhuru pasipo na safari hairuhusiwi, hivyo ikalazimika iruhusiwe kukusanya kwa ajili ya udhuru wa safari, mvua na udhuru mwingine."[41]

Aliyoyahakiki Ar-Razi katika mada hii ni ukweli mtupu, lakini kuiacha kwake haki kwa hoja ya: 'Hakika kukusanya bila udhuru wowote pasipo na safari hairuhusiwi kwa kuwa kuna dalili juu ya hilo,' ni dhana tu.

Ni dalili ipi iliyopo inayokataza kukusanya bila udhuru wowote, je, dalili ni Kitabu cha Mwenyezi Mungu? Huku Kitabu kwa mujibu wa uhakiki wake kinaruhusu kukusanya. Au ni Sunna? Baada ya muda utaona jinsi maelezo ya Sunna yanavyoruhusu.

Lakini pia umeshajua jinsi Masunni walivyosema kuwa inaruhusiwa, zaidi ya hapo ni kuwa Maimamu wa Ahlul-Bayt nao wameruhusu. Hivyo baada ya Kitabu, Sunna na ijmai hakuna hoja nyingine kama ilivyo 'baada ya Abadan

41 *Tafsirul-Kabir*, Juz. 12, Uk. 27

hakuna kijiji kingine.’[42]

## Kukusanya Sala mbili bila udhuru usipokuwa safarini kwa mujibu wa Sunna

Kuna riwaya nyingi zinazodhihirisha haki kuhusu ruhusa ya kukusanya Sala mbili bila udhuru pasipokuwa safarini, riwaya hizo zimepokewa na waandishi wa Sahih sita, Sunan na Masanidi. Hivyo tuanze aliyopokea Muslim kwa sanadi na tamko kisha twende kwenye yale waliyonukuu wengine.

1. Ametuhadithia Yahya mwana wa Yahya amesema: Nilisoma kwa Malik toka kwa Zuberi toka kwa Said bin Jubair toka kwa Ibnu Abbas alisema: ‘Mtume aliswali Adhuhuri na Al-Asr pamoja, Magharibi na Isha pamoja bila ya hofu wala safari.”

42 Mara ngapi Imam Ar-Razi amehakiki na kuongea lile lililo haki ambalo yeye mwenyewe anastahiki kulifuata lakini huliacha kwa hoja ya kipuuzi. Angalia aliyoyahakiki kuhusu kupaka miguu miwili katika tafsiri ya: “Na mpake vichwa vyenu na miguu yenu mpaka vifundoni.” Na yale aliyozungumza kuhusu makusudio ya “Wenye mamlaka katika ninyi” katika tafsiri ya Aya: “Mtiini Mwenyezi Mungu na mtiini Mtume na wenye mamlaka katika nyinyi". Na sehemu nyingine kama hizi.

2. Ametusimulia Ahmad bin Yunus na Aun bin Salam wote toka kwa Zuhayri, Ibnu Yunus alisema: "Ametusimulia Zuhayri, ametusimulia baba Zuberi toka kwa Saidi bin Jubair toka kwa Ibnu Abbas` alisema: 'Mtume aliswali Adhuhuri na Al-Asr pamoja Madina pasi na hofu wala safari.' Baba Zuberi akasema: 'Nikamuuliza Said, kwa nini alifanya hivyo? Akajibu: Nilimuuliza Ibnu Abbas kama ulivyoniuliza akasema: 'Alitaka asimpe taabu yeyote katika umma wake.'"

3. Ametusimulia Abu Bakr bin Abi Shaybat na Abu Kuraybi wamesema: Ametusimulia Abu Muawiya na ametusimulia Abu Kuraybi na Abu Said Al-Ashaju (tamko ni la Abu Kuraybi) walisema: 'Alitusimulia Wakiu wote kutoka kwa Al-A'amash toka kwa Habibu bin Abi Thabit, toka kwa Said bin Jubairi toka kwa Ibnu Abbas alisema: 'Mtume wa Mwenyezi Mungu alikusanya Adhuhuri na Al-Asr, Magharibi na Isha Madina pasi na hofu wala mvua.'

Katika hadith ya Wakiu amesema: Nikamwambia Ibnu Abbas: Kwanini alifanya hivyo? Akasema: Ili asiupe taabu umma wake. Katika Hadithi ya Abu Muawiya ni kuwa Ibnu Abbas` aliambiwa: Alitaka nini katika hilo?

Akasema: Ili asiupe taabu umma wake.

Ametusimulia Abu Bakr bin Shaybat, ametusimulia Sufiani bin Uyayna toka kwa Amru toka kwa Jabiri bin Zaidi toka kwa Ibnu Abbas alisema: "Niliswali na Mtume wa Mwenyezi Mungu rakaa nane pamoja na saba pamoja. Nikasema: Ewe baba As-sha'shau, nadhani alicheleweshaAdhuhuri na akaharakisha Al-Asr, akachelewesha Magharibi akaharakisha Isha. Akasema: "Na mimi nadhani hivyo."[43]

Kama atakusudia kukusanya kwa kimuonekano basi dhana yake si kitu haisaidii haki chochote. Muda si mrefu utakufikia ufafanuzi kuhusu kukusanya kimuonekano.

Ametusimulia Abu Rabiu Az-Zaharany, ametusimulia Hamadi bin Zaid toka kwa Amru bin Dinari toka kwa Jabiri bin Zaid toka kwa Ibnu Abbas kuwa, Mtume aliswali Madina rakaa saba na nane,[44] Adhuhuri na Al-Asr, Magharibi na Isha.

43 Kwa alama ya hadith ya tano ni kuwa Mtume alifanya hivyo alipokuwa Madina.

44 Kutaja bila kufuata mpangilio kwani mpangilio ni nane na saba

Amenisimulia Abu Rabiu Az-Zaharany. Ametusimulia Hamadi toka kwa Zuberi bin Al-Khariti toka kwa Abdallah bin Shaqiqi alisema: "Siku moja Ibnu Abbas alitutolea muhadhara baada ya Al-Asr mpaka lilipokuchwa jua na nyota zikaanza kuonekana. Watu wakawa wanasema: Sala! Sala! Mara akaja mtu mmoja wa koo ya Bani Tamim huku akisisitiza: Sala! Sala! Ndipo aliposema Ibnu Abbas: "Je unanifundisha Sunna? Usiye na mama wee! Kisha akasema: 'Nilimuona Mtume amekusanya Sala ya Adhuhuri na Al-Asr, na Magharibi na Isha.' Abdallah bin Shaqiqi anasema: 'Hilo likanitia shaka moyoni mwangu, mara moja nikaenda kwa Abu Huraira nikamuuliza, naye akathibitisha habari ya Ibnu Abbas kuwa ni kweli."

Ametusimulia Ibnu Abi Omar. Ametusimulia Wakiu. Ametusimulia Amrani bin Hudayri toka kwa Abdallah bin Shaqiq Al-Uqayliy amesema: Mtu mmoja alimwambia Ibnu Abbas: "Sala!" Akanyamaza. Kisha akasema: "Sala!" Akanyamaza. Kisha akasema: "Sala!" Akanyamaza. Kisha akasema: "Ee usiye na mama we!" Unatufunza Sala ilhali tulikuwa tukikusanya kati ya Sala mbili zama za Mtume wa Mwenyezi Mungu.[45]

Haya ndiyo aliyoyanukuu Muslim ndani ya *Sahih* yake. Yafuatayo ni waliyonukuu wengine.

Ametoa Bukhari toka kwa Ibnu Abbas kuwa: "Mtume aliswali Madina saba na nane pamoja, Adhuhuri na Al-Asr, Magharibi na Isha. Ayubu akasema: 'Huenda alikuwa ndani ya usiku wa mvua.' Akasema, huenda."[46]

Ametoa Bukhari toka kwa Jabiri bin Zaidi toka kwa Ibnu Abbas amesema: "Mtume aliswali saba pamoja na nane pamoja."[47]
Ametoa Bukhari kwa kuivusha toka kwa Ibnu Omar na

45 Sherhe ya *Sahih Muslim* ya An-Nawawiy Juz. 5 Uk. 213-218. Mlango wa kukusanya Sala usipokuwa safarini. Japokuwa huu ni mlango mahususi kwa ajili ya riwaya za kukusanya usipokuwa safarini lakini kanukuu riwaya tatu zinazoonyesha kukusanya Sala mbili safarini hivyo hatujazinukuu. Inawezekana aliziweka riwaya hizi katika mlango huu ili kuonyesha kuwa kukusanya katika hali isiyo ya safari ni vilevile kama unavyokusanya safarini

46 *Sahih Bukhari*, Juz. 1, Uk. 110 Kitabu cha Sala mlango wa kuchelewesha *Sahih Bukhari*: Juz.1 Uk. 113, Kitabu cha Sala mlango wa wakati wa Magharibi.

47 *Sahih Bukhari*: Juz.1 Uk. 113 Kitabu cha Sala mlango wa wakati wa Magharibi.

Abi Ayyub na Ibnu Abbas kuwa: Mtume aliswali Magharibi na Isha.[48]

Ametoa Tirmidhiy toka kwa Saidi bin Jubairy toka kwa Ibnu Abbas alisema: Mtume alikusanya kati ya Adhuhuri na Al-Asr na kati ya Magharibi na Isha Madina pasi na hofu yoyote wala mvua. Akasema: Akaambiwa Ibnu Abbas: 'Alitaka nini katika hilo?' Akasema: 'Alitaka asiupe taabu umma wake.' Baada ya kunukuu Hadithi hii Tirmidhy akasema: Hadithi ya Ibnu Abbas imepokewa toka kwake na watu zaidi ya mmoja, kaipokea Jabir bin Zaidi, Saidi bin Jubayri, na Abdallah bin Shaqiqi Al-Uqayliy. [49]

48 *Sahih Bukhari*: Juz.1 Uk. 113 mlango wa Isha

49 *Sunanut-Tirmidhy*: Juz.1, Uk. 354 Hadithi namba 187 mlango wa yanayozungumzia kukusanya usipokuwa safarini. Kisha angalia kuwa muhakiki kwenye ufafanuzi kataja njia za upokezi zilizopokea Hadithi hii toka kwa Ibnu Abbas. Pia *At-Tirmidhy* ana tafsiri isiyokubalika kuhusu Hadithi hii. Utaiona muda wake ukifika.

Imam Ahmad ameitoa toka kwa Qatada amesema: "Nilimsikia Jabir bin Zaidi toka kwa Ibnu Abbas akisema: Mtume wa Mwenyezi Mungu alikusanya kati ya Adhuhuri na Al-Asr, Magharibi na Isha Madina pasipo na hofu wala mvua.' Ibnu Abbas akaulizwa: 'Alitaka nini kinyume na hayo?' Akasema: 'Alitaka asiupe taabu umma wake.'[50]

Imam Ahmad ametoa toka kwa Sufiyani amesema Umar: Amenipa habari Jabir bin Zaidi kuwa alimsikia Ibnu Abbas akisema: Niliswali na Mtume wa Mwenyezi Mungu nane pamoja na saba pamoja. Nikamwambia: 'Ewe Abu Shauthau, nadhani alichelewesha Adhuhuri na akaharakisha Al-Asr, Akachelewesha Magharibi akaharakisha Isha. Akasema: Nami nadhania hivyo."[51]

14. Imamu Ahmad ametoa toka kwa Abdallah bin Shaqiqi alisema: "Siku moja Ibnu Abbas alitutolea muhadhara baada ya Al-Asr mpaka lilipokuchwa jua na nyota zikaan-

50 *Musnad Ahmad,* Juz. 1, Uk. 223

51 *Musanad Ahmad* Juz.1, Uk. 221 alidhania kuwa alikusudia kukusanya kimuonekano. Dhana hii si hoja hata kwa yeye mwenyewe mdhaniaji. Dhana haisaidii haki chochote

za kuonekana. Watu wakakawa wanasema: "Sala! Sala! Alikuwepo mtu mmoja wa ukoo wa Bani Tamimu akaanza kusema: Sala Sala! Ibn Abbas akaghadhibika akasema: Je unanifundisha Sunna? Nilimuona Mtume amekusanya baina ya Adhuhuri na Al-Asr, na Magharibi na Isha. Abdallah anasema: Hilo likanitia shaka moyoni mwangu, mara moja nikaenda kwa Abu Huraira nikamuuliza, akalikubali.[52] (1)

Ametoa Malik toka kwa Saidi bin Jubairy toka kwa Abdallah bin Abbas kuwa alisema: "Mtume wa Mwenyezi Mungu aliswali Adhuhuri na Al-Asr zote pamoja, Magharibi na Isha zote pamoja pasipo na hofu wala safari."[53]

Ametoa Abu Daudi toka kwa Saidi bin Jubairy toka kwa Abdallah bin Abbas` amesema: Mtume wa Mwenyezi Mungu aliswali Adhuhuri na Al-Asr zote pamoja, Magharibi na Isha zote pamoja pasipo na hofu wala safari.

52 *Musnad* ya Ahmad Juz. 1, Uk. 151

53 *Muwatta* ya Malik Juz.1, Uk. 144 Hadithi ya 4 mlango wa kukusanya Sala safarini na pasipo safari.

Malik akasema: Mimi naona alifanya hivyo wakati wa mvua.(3)

Abu Daudi ameitoa toka kwa Jabiri bin Zaidi toka kwa Ibnu Abbas alisema: "Mtume wa Mwenyezi Mungu alituswalisha Madina nane na saba, Adhuhuri na Al-Asr, Magharibi na Isha. Abu Daudi akasema: Ameipokea pia Swaleh bwana wa At-Tauamah toka kwa Ibnu Abbas akasema: 'Pasipo na mvua."[54]

Ametoa An-Nasai toka kwa Saidi bin Jubair toka kwa Ibnu Abbas kuwa: "Mtume wa Mwenyezi Mungu aliswali Adhuhuri na Al-Asr zote pamoja, Magharibi na Isha zote pamoja pasipo na hofu wala safari."[55]

Ametoa An-Nasai toka kwa Saidi bin Jubair toka kwa Ibnu Abbas kuwa: Mtume alikuwa akiswali Madina akikusanya kati ya Sala mbili kati ya Adhuhuri na Al-Asr, Magharibi na Isha bila ya hofu wala safari. Akaambiwa:

---

54 Rejea iliyopita, Hadith Na, 1214

55 *Sunanun-Nasai*, Juz. 1 Uk. 290 mlango wa kukusanya Sala mbili usipokuwa safarini.

Kwa nini? Akasema: Ili asiupe taabu umma wake." (3) Ametoa An-Nasai toka kwa Abi Shauthau toka kwa Ibnu Abbas amesema: "Niliswali nyumma ya Mtume wa Mwenyezi Mungu nane zote pamoja na saba zote pamoja."[56]

Ametoa An-Nasai toka kwa Jabir bin Zaidi toka kwa Ibnu Abbas kuwa aliswali huko Basra Sala ya mwanzo na Al-Asr bila ya kitu kati yake, na Magharibi na Isha bila ya kitu kati yake. Alifanya hivyo kutokana na shughuli. Na Ibnu Abbas akadai kuwa Aliswali na Mtume wa Mwenyezi Mungu Madina Sala ya mwanzo na Al-Asr sijida nane bila ya kitu kati yake.[57]

Hafidh Abdu Razaqi toka kwa Daudi bin Qaysi toka kwa Swaleh bwana wa At-Tauamah kuwa alimsikia Ibnu Abbas akisema: "Mtume wa Mwenyezi Mungu alikusanya kati ya Adhuhuri na Al-Asr, Magharibi na Isha

56 *Sunanun-Nasai*, Juz.1 Uk. 290 mlango wa kukusanya Sala mbili usipokuwa safarini.

57 *Sunanun-Nasai*, Juz.1 Uk. 286 mlango: Wakati ambao asiye safarini hukusanya Sala, na makusudio ya sijida

Madina pasipo na safari wala mvua.” Akasema: ‘Nikamwambia Ibnu Abbas: Unadhani kwa nini alifanya hivyo?’ Akasema: ‘Ninaona ili aupe nafuu umma wake.”[58]

Ametoa Abdu Razaqi toka kwa Ibnu Abbas amesema: “Mtume wa Mwenyezi Mungu alikusanya kati ya Adhuhuri na Al-Asr Madina pasipo na safari wala hofu. Akasema: ‘Nikamwambia Ibnu Abbas, unaona ni kwa nini alifanya hivyo? Akasema: ‘Alitaka asimpe yeyote taabu katika umma wake.”[59]

Ametoa Abdu Razaqi toka kwa Amru bin Dinari kuwa Aba As-Shauthau alimpa habari kuwa Ibnu Abbas` alimueleza akasema: ‘Niliswali nyuma ya Mtume nane zote pamoja na saba zote pamoja Madina. Ibnu Jarihu akasema: ‘Nikamwambia Abu Shauthau mimi nadhani Mtume alichelewesha Adhuhuri kidogo akatanguliza Al-Asr kidogo. Abu Shaathau akasema: “Na mimi nadhania

58 1-2- *Muswanafu Abdu-Razaqi*, Juz. 2 Uk. 555-556 Hadithi ya 4434, 4435.

59 1-2- *Muswanafu Abdu-Razaqi*, Juz. 2 Uk. 555-556 Hadithi ya 4434, 4435.

hivyo."**[60]**

Nasema: Dhana ya Ibnu Jarihu si chochote japo Abu Shauthau ameiafiki, dhana haisaidii haki chochote. Matokeo yake ni kuwa kukusanya kulikuwa ni kimfano si kihalisi, hivyo tutakubainishia udhaifu wa maana hii ya kukusanya kimuonekano, na kuwa kukusanya kimuonekano kunawajibisha taabu zaidi kuliko kutenganisha, kwani kujua mwisho wa wakati wa Sala ya mwanzo na mwanzo wa Sala ya pili ni taabu zaidi kuliko kukusanya.

Abdu Razaqi ametoa toka kwa Amru bin Shuaybu toka kwa Abdallah bin Omar amesema: "Mtume wa Mwenyezi Mungu alitukusanyia bila ya kuwa safarini akakusanya Adhuhuri na Al-Asr." Mtu mmoja akamwambia Ibnu Omar: "Unaona ni kwa nini Mtume alifanya hivyo." Akajibu: "Ili umma wake usipate taabu iwapo mtu akikusanya."**[61]**

---

60 *Muswanafu Abdu-Razaqi*: Juz. 2, Uk. 556 Hadithi ya 4436

61 *Muswanafu Abdu-Razaqi*, Juz. 2 Uk. 556 Hadithi ya 4437

At-Twahawiy ndani ya kitabu *Maanil-athari* amesema toka kwa Jabir bin Abdallah: "Mtume wa Mwenyezi Mungu alikusanya kati ya Adhuhuri na Al-Asr, Magharibi na Isha Madina kwa hiyari bila ya hofu wala ila." [62]

Al-Hafidh Abu Naiimu Ahmad bin Abdallah Al-Isfihaniy (aliyefariki mwaka 430 A.H.) ametoa toka kwa Jabir bin Zaidi kuwa Ibnu Abbas alikusanya kati ya Adhuhuri na Al-Asr, na akadai kuwa yeye aliswali na Mtume Madina Adhuhuri na Isha.[63]

Abu Naiimiy ametoa toka kwa Amru bin Dinari amesema: "Nilimsikia Abu Shauthau akisema: "Ibnu Abbas` amesema: "Mtume wa Mwenyezi Mungu aliswali rakaa nane zote pamoja, na rakaa saba zote pamoja bila ya ugonjwa wala udhuru."[64]

Ametoa Al-Bazari ndani ya *Musnadi* yake toka kwa Abu Hurayra kuwa alisema: "Mtume wa Mwenyezi Mungu

---

62 *Maanil-Athari*, Juz.1, Uk. 161

63 *Hil-yatul-Awliyai*, Juz. 3, Uk. 90 mlango wa Jabir bin Zaid

64 *Hulyatul-Awliya*, Juz. 3, Uk. 90 mlango wa Jabir bin Zaid

alikusanya kati ya Sala mbili Madina bila ya hofu."[65]

At-Tabaraniy ametoa ndani ya kitabu *Al-Awsatu* na *Al-Kabiri* toka kwa Abdallah bin Zaid kuwa Mtume wa Mwenyezi Mungu alikusanya Adhuhuri na Al-Asr, Magharibi na Isha. Akaulizwa kuhusu hilo akajibu: "Nimefanya hivyo ili nisiupe taabu umma wangu." [66]

Hizi ni Hadithi thelathini tumezikusanya toka kwenye *Sahih Sita, Masnadi* na *Sunnani*.

Tumefupisha maneno kwa kutoa riwaya hizi tu ili msomaji ajue kuwa ni Hadithi ambazo wanazuoni wa Hadithi na wakubwa wao wamezitilia umuhimu hivyo wakazihifadhi, na wala mtu hawezi kuzikataa na kuzikanusha. Na kuna riwaya nyingize zaidi ya hizi hatujazitaja kwa ajili ya kufupisha.[67]

Mtiririko huu wa wapokezi unakomea kwa watu wafu-

---

65 *Musnadul-Bazari*, Juz. 1, Uk. 283 Hadithi namba 412

66 *Al-Muujamul-Kabiri* Juz.10, Uk. 269 Hadithi ya 10525

67 Angalia *Al-Maujamul-Awsatu*, Juz. 2, Uk. 94. *Kanzul-Ummal*, Juz.8 Uk.246-251 namba 22764, 22767, 22771, 22774, 22777, 22778.

atao:
Abdallah bin Abbas
Abdallah bin Omar
Abu Ayubu Al-Annswariy mwenyeji wa Mtume Madina
Abu Hurayra Ad-Duusiy
Jabiri bin Abdillah Al-Answariy
Abdallah bin Mas'udi.

Riwaya zinaeleza wazi kuwa Mtume wa Mwenyezi Mungu alikusanya Madina kati ya Sala mbili pasipo na hofu, mvua wala sababu yoyote. Alikusanya ili kubainisha ruhusa ya kukusanya na kuwa kufanya hivyo ni sheria. Pia ili mtu asije akadhani kuwa kutenganisha ni lazima kutokana na yeye Mtume kuendelea kuswali ndani ya wakati wa ubora. Hivyo kwa kitendo chake cha kukusanya kimethibitisha kuwa kukusanya ni ruhusa japokuwa kutenganisha ni bora.

Kwa kuwa madhumuni ya riwaya yanapingana na madhehebu za kifiqhi zilizozoweleka hivyo baadhi ya watu wa Hadithi na wanazuoni wa fiqhi wamejaribu kuzilazimisha riwaya zifuate fat'wa za maimamu zao na kufanya fat'wa hizo ndio kipimo cha haki na batili.

Hivyo wengi wao wakaacha kuzitumia riwaya hizi isipokuwa wachache tu ndio waliozitumia wakatoa fat'wa kulingana na madhumuni ya riwaya, hao wametajwa majina yao na Ibnu Rushdi ndani ya kitabu chake *Bidayatul-Mujtahidu*. Na Wametajwa na An-Nawawiy ndani ya *Al-Maj'muu* kama ilivyotangulia.

Na kifuatacho ni sababu na nyudhuru walizozitoa waliokhalifu riwaya, nazo ni sababu na nyudhuru dhaifu kuliko nyumba ya buibui.

## Wanazuoni wengi wa kisunni wameacha kuifanyia kazi

Hakika kati ya mambo yanayozisibu riwaya hizi ni wanazuoni wengi wa kisunni kuacha kuzitumia, jambo ambalo linawajibisha zisiwe na hoja.

Baada ya kutaja Hadithi za kukusanya, Tirmidhiy anasema: Kuzifanyia kazi hizi riwaya kwa masunni ni kutokukusanya kati ya Sala mbili isipokuwa safarini au Arafa. [68]

[68] *Sunanut-Tirmidhiy*, Juz.1, Uk. 354

Watafiti wengi wa dini wameijibu kauli hii:
a). An-Nawawiy anasema: "Riwaya hizi zimethibiti ndani ya *Muslim* kama unavyoziona. Na wanazuoni wana tafsiri na madhehebu mbalimbali kuhusu riwaya hizi, na Tirmidhiy mwisho wa kitabu chake amesema: Ndani ya kitabu changu hakuna Hadithi ambayo umma umeafikiana juu ya kuiacha na kutokuifanyia kazi isipokuwa Hadithi ya Ibnu Abbas inayohusu kukusanya Madina bila ya hofu wala mvua, na Hadithi ya kumuua mnywaji wa pombe mara ya nne."[69]

Hili alilolisema Tirmidhiy kuhusu Hadithi ya mnywaji wa pombe ndivyo lilivyo, yenyewe ni Hadithi iliyofutwa kwani ijmai imethibitisha hilo. Ama kuhusu Hadithi ya Ibnu Abbas hakuna ijmai inayothibitIsha kuacha kuifanyia kazi, isipokuwa kuna baadhi ya tafsiri ambazo tutaziashiria.[70] (1)

b). As-Shaukaniy amemjibu At-Tirmidhiy kwa kusema: "Haijifichi kuwa Hadithi ni Sahih, na wala kitendo cha

69 Taz. *Al-Ilali*, Juz. 2, Uk. 331 na Juz. 4, Uk. 384

70 *Sharh ya Sahih Muslim* ya An-Nawawiy Juz. 5 Uk. 224

masunni wengi kuacha kuifanyia kazi hakitii dosari usahihi wake, na wala hakiwajibishi kuporomoka hoja yake. Baadhi ya wanazuoni wameifanyia kazi kama ilivyotangulia. Japokuwa dhahiri ya maneno ya Tirmidhiy ni kuwa yeye haifanyii kazi lakini wengine wamethibitisha kuifanyia kazi, na kilichothibitishwa hutangulizwa.[71]

c). Al-Alusiy amesema: "Madhehebu ya kundi la maimamu linaruhusu kukusanya usipokuwa safarini kwa mwenye haja asiyefanya kuwa ni mazowea. Kauli hii ndiyo ya Ibnu Sirini, na Ash'habu mfuasi wa Malik.

Al-Khatabiy Ameinukuu toka kwa Al-Qufali As-Shashiy Al-Kabiru mfuasi wa Imam Shafy, na kutoka kwa Abi Is'haqa Al-Marwaziy na toka kwa jamaa kati ya watu wa Hadithi.

Ibnu Al-Mundhiru amechagua kauli hii, na inaungwa mkono na dhahiri iliyosihi toka kwa Ibnu Abbas` na iliyopokewa na Muslim kuwa alisema: Mtume wa Mwenyezi Mungu alikusanya kati ya Adhuhuri na Al-Asr, Magharibi

71 *Naylul-Awtwari* ya As-Shawkaniy Juz. 3, Uk. 218 mlango wa kukusanya kwa asiye msafiri kwenye mvua au kingine.

na Isha Madina pasipo na hofu wala mvua. Akaambiwa: Kwa nini amefanya hivyo? Akasema: "Hakutaka yeyote apate taabu katika umma wake."

Inatokana na taabu kwa maana ya uzito hivyo hajatoa sababu ya ugonjwa wala ya kitu kingine.

Kutokana na tuliyoyataja inafahamika kuwa kauli ya At-Tirmidhiy mwishoni mwa kitabu chake: Ndani ya kitabu changu hakuna Hadithi ambayo umma umeafikiana juu ya kuiacha na kutokuifanyia kazi isipokuwa Hadithi ya Ibnu Abbas inayohusu kukusanya Madina bila ya hofu wala mvua, na Hadithi ya kumuua mnywaji wa pombe mara ya nne. Inatokana na kutokufanya utafiti .

Ndio! Aliyoyasema kuhusu Hadithi ya pili ni sahihi kwani wameeleza wazi kuwa Hadithi hiyo imefutwa na ijmai imethibitisha kufutwa kwake.[72] (1)

d). Kwa ukosoaji huu imedhihirika kuwa hakuna hali ya kususa kuifanyia kazi Hadithi hii, na huenda masunni

72 *Ruhul-Maaniy*, Juz. 15 Uk. 133-134 katka tafsiri ya Aya: "Simamisha Sala jua linapopinduka"

wengi hawajatoa fat'wa kulingana na makusudio ya Hadithi hizi kwa sababu ya ubora wa kutenganisha na kuzigawa kwa nyakati.

Lakini ubora huu unapingana na ubora mwingine, nao ni kuwa katika zama zetu hizi kitendo cha kutenganisha kinapelekea watu wengi wenye shughuli kuacha kuswali (kama tunavyoshuhudia kwa macho). Kinyume na kukusanya kwenyewe ambako kunarahisisha kuhifadhi Sala kwa kuziswali, kwa ajili hiyo ubora umegeukia upande wa pili, hivyo ni bora wanazuoni wa sheria wakatoa fat'wa ya kukusanya, na watie wepesi badala ya kutia uzito.

Allah (s.w.t.) anasema: "Mwenyezi Mungu huwatakieni yaliyo mepesi wala hawatakieni yaliyo mazito."[73] "Wala hakuweka juu yenu uzito katika dini."[74]

Tunamshukuru Mwenyezi Mungu kwani zipo dalili zinazoruhusu kukusanya katika hali yoyote, tena ni dalili sahi-

73 Al-Baqara: 185

74 Al-Hajji: 78

hi na za wazi kama ulivyoona, bali ni Kitabu chenye hekima ndio kimebainisha hivyo.[75]

**2. Hadithi haielezi kukusanya kwa kutanguliza au kwa kuchalewesha.**

Al-Qadhiy Sharafudini Al-Husein bin Muhammad Al-Maghribiy amesema ndani ya kitabu chake *Al-Badru At-Tamamu fi sharhu Bulughul-Marami* kuwa: "Hakika Hadithi ya Ibnu Abbas haisihi kuwa hoja kwa sababu haiainishi ni kukusanya kwa kutanguliza au ni kwa kucheleweshа, hiyo ni kama ilivyo dhahiri katika riwaya ya Muslim na kuainisha moja kati ya hizo ni kulazimisha. Hivyo inawajibika kuhama kwenda kwenye lile la wajibu kwa kubakia katika Hadithi za nyakati zinazomjumuisha mwenye udhuru na asiye na udhuru kisha kumuainisha msafiri tu kwa kuthibiti kiainishi.[76]

Anajibiwa kuwa: Ibnu Abbas hakunukuu namna ya kukusanya kwa kuwa jambo lenyewe liko wazi, kwani kuku-

75 *Masailul-Fiqihiya* ya Imam Sharaful-dini: 9

76 Ameelezea As-Sayyid Muhammad bin Ismail As-Swanaaniy ajulikanae kwa jina la Al-Amiru ndani ya kitabu chake *Subulus-Salami*: Juz. 2, Uk. 43

sanya katika hali isiyo ya safari ni sawa na kukusanya katika hali ya safari, hivyo kama inavyoruhusiwa kukusanya kwa namna zote mbili uwapo safarini yaani kukusanya kwa kutanguliza na kwa kuchelewesha kama maelezo yalivyotangulia ndivyo hivyo hivyo hata usipokuwa safarini.

Kunyamaza kwa Ibnu Abbas na kitendo cha wapokezi kutokumuuliza kuhusu namna ya kukusanya ni dalili kuwa kutokana na maneno yake walifahamu kukusanya si mahususi kwa namna moja tu kati ya namna mbili, kwani laiti isingekuwa hivyo ingewalazimu kuuliza tena: Je, Mtume alikusanya kwa namna ya kutanguliza au kuchelewesha?

Linalounga mkono hilo ni umoja wa sababu iliyopo kwenye maneno ya Ibnu Abbas kwani inapatikana katika namna zote mbili.

Ametoa Muslim toka kwa Ibnu Abbas kuwa Mtume wa Mwenyezi Mungu alikusanya Sala mbili katika safari aliyosafiri katika vita vya Tabuk, hivyo akakusanya kati ya Adhuhuri na Al-Asr, Magharibi na Isha. Said akasema:

‘Nikamwambia Ibnu Abbas kitu gani kilimpelekea kufanya hivyo, akasema: “Alitaka asiupe taabu umma wake.”[77]

Hivyo kinachoupa nguvu uhusikaji wa namna zote mbili bila tofauti kati ya namna hizo ni kule kuenea kwa sababu nayo ni kuuondolea taabu umma wake, kwani kwa hakika taabu inayopatikana kwa kutenganisha Sala mbili inaondoka kwa kukusanya kwa namna yoyote ile kati ya namna mbili. Sawa iwe kwa kutanguliza au kuchelewesha.

Zaidi ya hapo ni kuwa Ibnu Abbas aliifanyia kazi Hadithi kwa sura ya kukusanya kwa kuchelewesha. Imeshatangulia kuwa Ibnu Abbas siku moja alihutubia baada ya Al-Asr mpaka jua likazama na nyota zikachomoza; watu wakaanza kusema: ‘Sala! Sala!’ Akaja mtu toka ukoo wa Bani Tamimu akaanza kusisitiza kwa kusema: ‘Sala! Sala!’ Ibnu Abbas akasema: “Je unanifundIsha sunna? Ee usiye na mama we!" Mpaka mwisho wa Hadithi kama ilivyotangulia.

Kwa hakika ndugu msomaji ni kuwa mpinzani alipofika

[77] Sharhu ya *Sahih Muslim* ya An-Nawawiy, Juz. 5, Uk. 224 mlango wa kukusanya Sala mbili Hadithi ya 51

mbele ya riwaya hizi nyingi zinazoruhusu kukusanya dhidi ya kutenganiha, kisha akaona wanazuoni wengi wako kinyume basi kwa makusudi akaanza kushakia, na kwa ajili hiyo akaleta utata huu ambao unafanana na swali la Bani Israeli kwa Nabii Musa bin Imran kuhusu miaka na rangi ya ng'ombe jike.[78]

## Alikusanya sala mbili kimuonekano

Wengi wanaojaribu kutatua suala hili hukimbilia kudai kuwa haikuwa ni kukusanya kwa halisi kama kukusanya kwa safarini, bali ilikuwa ni kukusanya kwa kimuonekano, yaani Mtume alichelewesha Adhuhuri mpaka ulipobakia muda wa rakaa nne ndipo akaswali Adhuhuri na baada ya kumaliza tu ukawa umeingia wakati wa Al-Asr akaswali Al-Asr, hivyo akawa kakusanya Sala mbili huku akiwa kaswali kila moja ndani ya wakati wake.

Hili ndilo linalodhihirika toka kwa wengi wanaofafanua Hadithi; na yafuatayo ni maelezo yao:
An-Nawawiy amesema: "Wapo waliofasiri kuwa ni

78 Al-Baqarat; 2: 67-71

kucheleweshа ya mwanzo mpaka mwisho wa wakati wake kisha aiswali ndani ya wakati wake, hivyo baada ya kumaliza ukawa umeingia wakati wa Sala ya pili akaiswali, hivyo Sala yake ikawa katika muonekano wa kukusanya."

Kisha akapinga akasema: "Kauli hii nayo ni dhaifu au batili kwa sababu inapingana na dhahiri kwa namna isiyotegemewa. Kwa sababu kitendo cha Ibnu Abbas tulichokitaja katika hotuba kisha kutoa kwake Hadithi kama hoja ya usahihi wa kitendo chake, kisha kuthibitisha kwake Abu Huraira bila kukanusha ni hoja tosha katika kupinga tafsiri hii.[79]

An-Nawawiy alipasa amjibu kwa hoja tuliyoitaja nayo ni kuwa: Mtume alikusanya Sala mbili kwa lengo la kuondolea umma wake taabu, na kukusanya kwa namna hiyo iliyotajwa kunataabisha zaidi kuliko kutenganisha.

Ibnu Quddama amesema: "Kukusanya ni hiyari, hivyo ingekuwa kukusanya ni kwa namna waliyoielezea basi ingekuwa ni taabu zaidi kuliko kuiswali kila Sala wakati

[79] Sharhu ya *Sahih Muslim*, Juz. 5, Uk. 225

wake. Kwa sababu kuiswali kila Sala wakati wake ni wepesi zaidi kuliko kulinda mwisho wa wakati, mwisho ambao unalingana na muda wa kuswali Sala ya mwanzo tu bila wakati kubaki.

Pia laiti kukusanya kungekuwa ni kwa namna hiyo basi ingeruhusiwa kukusanya kati ya Al-Asr na Magharibi na Isha na Asubuhi. Ilihali hakuna tofauti kati ya umma kuwa kufanya hivyo ni haramu. Hivyo kuzifanyia kazi riwaya kwa ufahamu uliyo karibu ni bora zaidi kuliko kulazimisha maana hiyo.[80] (1)

Pia Al-Muqaddasiy ndani ya kitabu *As-Sharhu Al-Kabiru* [81] amejibu tafsiri hii kama alivyojibu Ibnu Quddama, tamko ni moja katika vitabu vyote viwili hivyo ndio maana tumetosheka na tamko la Ibnu Quddama.

Ndio, Kulingana na tuliyonukuu toka kwao ni kuwa wao wamemjibu yule aliyefasiri ruhusa ya kukusanya Sala

80 *Al-Mughni*, Juz. 2, Uk. 113-114 ameitaja alipokuwa akikosoa maneno ya yule aliyefasiri maana hii katika kukusanya kwa safarini. Hivyo kwa kuwa jambo ni moja ndio maana tumeitaja hapa.

81 *As-Sharhul-Kabiru fi Dhaylil-Mughniyi*, Juz. 2, Uk. 115

mbili kwa msafiri kwa tafsiri ya kukusanya kimuonekano.

Hivyo kwa kuwa sababu ya kukusanya katika hali zote mbili (Msafiri na asiye msafiri) ni moja, nayo ni kuuondolea umma wake taabu na uzito huku kukusanya kwa muonekano kukiwa ni taabu na uzito zaidi kuliko kutenganisha basi tunathibitisha maneno yao katika mada hii. (Kukusanya bila udhuru katika hali isiyo ya safari).

Dhahiri ni kuwa jina kukusanya, kijamii halimlengi mtu aliyecheleweshа Adhuhuri akaja kuiswali mwisho wa wakati wake na akaiharakisha Al-Asr akaiswali mwanzo wa wakati wake, kwa sababu huyu kaswali kila Sala ndani ya wakati mahususi kwa Sala husika.

Amesema: "Hakika kukusanya kunakojulikana ni kuswali Sala zote mbili pamoja ndani ya wakati wa mojawapo, hivi huoni kukusanya Sala mbili Arafa na Muzdalifa ndivyo kulivyo?"[82]

---

**82** *Maalimus-Sunan*, Juz. 2 Uk. 53 Hadithi ya 1163, *Aunul-Maabudu*, Juz. 1, uk. 468.

## Dalili za As-Shaukaniy za kuthibitisha kuwa kukusanya kulikuwa kwa kimuonekano

Kisha As-Shaukaniy ni kati ya watu wanaounga mkono kuwa kukusanya kulikuwa ni kwa kimuonekano. Ameunga mkono hilo kwa hoja tatu:

Ya kwanza: Riwaya aliyoitoa Malik katika *Al-Muwatwau* na Bukhari, Abu Daud na An-Nasaiy toka kwa Ibnu Mas'udi kuwa alisema: "Sikumuona Mtume akiswali Sala nje ya wakati wake isipokuwa Sala mbili alikusanya Magharibi na Isha Muzdalifa na siku hiyo akaswali alfajiri kabla ya wakati wake."

As-Shaukaniy akasema: Ibnu Mas'ud kakataa namna yoyote ya kukusanya na akaihusisha na kukusanya Muzdalifa tu, japokuwa yeye mwenyewe ni kati ya watu waliyopokea kukusanya kwa Madina kama ilivyotangulia.

Hivyo inaonyesha kuwa kukusanya kulikofanyika Madina ni kukusanya kwa kimuonekano, kwani laiti ingekuwa ni kukusanya kwa halisi basi riwaya zake

zingepingana, na ni lazima tukusanye riwaya hizi kwa namna itakayowezekana. [83]

**Anajibiwa:**

Kwanza: Ibnu Mas'udi si hoja kwa sababu amehusisha kukusanya na Muzdalifa tu ilihali kuna riwaya nyingi zinazoonyesha kuwa Mtume alikusanya Muzdalifa na Arafa, hivyo dhahiri ya Hadithi hii inaachwa wala haitegemewi, wala haisihi kuwa alama ya kuainisha makusudio ya kukusanya katika riwaya za mada hii.

Pili: Ibnu Mas'udi mwenyewe amepokea kukusanya kwa Mtume Sala mbili Madina, na akasema: "Alikusanya Mtume wa Mwenyezi Mungu Adhuhuri na Al-Asr, Magharibi na Isha." Akaulizwa kuhusu hilo akasema: "Nimefanya hivyo ili umma wangu usitaabike." [84]

Umeshafahamu kuwa kukusanya kwa kimuonekano kunataabisha zaidi kuliko kukusanya kwa halisi, kwani kufahamu mwisho wa nyakati na mwanzo wake bila

83 *Naylul-Awtari min ahadithi Sayidul-Akhbari*, Juz. 3, Uk. 217

84 Angalia riwaya namba 30

kukosea ilikuwa ni tatizo kwa zama zilizopita hivyo hakuna njia isipokuwa ni kutafsiri kukusanya kwa maana ya kukusanya kwa uhalisia. Hii ni dalili kuwa riwaya inayohusisha kukusanya kwa Muzdalifa tu imeachwa na wala si hoja.

Ya pili: Aliyopokea Ibnu Jariri toka kwa Ibnu Umar amesema: "Mtume wa Mwenyezi Mungu alitujia akawa akicheleweshа Adhuhuri na kuharakisha Al-Asr hivyo anazikusanya pamoja. Anachelewesha Magharibi na anaharakisha Isha hivyo anazikusanya pamoja na huku ndio kukusanya kwa kimuonekano."[85]

Anajibiwa kuwa Hadithi hii japokuwa inahusisha kukusanya kwa kimuonekano lakini haichukuliwi kwa sababu muradi wake hauko wazi, kwani laiti akimaanIsha kuwa Mtume alifanya hivyo safarini basi imeshatangulia kuwa ukusanyaji wa Mtume safarini ulikuwa ni halisi.

Amepokea Muslim toka kwa Anas bin Malik kuwa alisema: "Ilikuwa Mtume akisafiri kabla ya kugeuka jua huchelewesha Adhuhuri mpaka wakati wa Al-Asr kisha

85 *Naylul-Awtari*, Juz. 3, Uk. 217

anashuka na kuzikusanya pamoja."[86]

Na katika riwaya nyingine toka kwake: "Hakika Mtume alikuwa aharakishwapo na safari huchelewesha Adhuhuri mpaka mwanzo wa wakati wa Al-Asr kisha anazikusanya pamoja, na anachelewesha Magharibi mpaka aje aikusanye na Isha mpaka wekundu wa Magharibi unapoondoka." [87]

Kama makusudio yake ni kuwa Mtume alikusanya kati ya Sala mbili kukusanya kwa kimuonekano ilihali hayupo safarini basi nadhani umeshajua jinsi riwaya zinazoonyesha ukusanyaji halisi zilivyonyingi, kiasi kwamba Hadithi ya Ibnu Abbas` na nyingine zimeweka wazi na ni alama tosha ya kutafsiri riwaya kwa maana ya ukusanyaji halisi, hivyo hatuwezi kuitupa Hadithi na kitendo cha Ibnu Abbas` eti kwa ajili ya Hadithi isiyokuwa wazi ya Ibnu Omar.

86 Sharhu *Sahih Muslim,* Juz. 5 mlango: Ruhusa ya kukusanya Sala mbili safarini. Namba 46 na 48

87 Sharhu *Sahih Muslim*, Juz. 5 mlango: Ruhusa ya kukusanya Sala mbili safarini. Namba 46 na 48

Ya tatu: Ameipokea An-Nasai toka kwa ibnu Abbas kuwa: Niliswali na Mtume Adhuhuri na Al-Asr pamoja, na Magharibi na Isha pamoja. Alichelewesha Adhuhuri akaharakisha Al-Asr, na akachelewesha Magharibi akaharakisha Isha. Na huyu ni Ibnu Abbas mpokezi wa Hadithi za mlango huu ametamka wazi kuwa aliyopokea kuhusu kukusanya ni kukusanya kwa kimuonekano.[88]

Anajibiwa kuwa: Tafsiri hii, yaani kauli: Alichelewesha Adhuhuri akaharakisha Al-Asr, na akachelewesha Magharibi akaharakisha Isha, si ya Ibnu Abbas bali ni ya Jabir bin Zaid, hiyo ni kwa alama ya Hadithi aliyoitoa Imam Ahmad toka kwa Jabir bin Zaid kuwa alimsikia Ibnu Abbas akisema: "Niliswali na Mtume wa Mwenyezi Mungu nane pamoja na saba pamoja. Nikamwambia, ewe Aba As-Shauthau nadhania alichelewesha Adhuhuri akaiharakisha Al-Asr na akachelewesha Magharibi akaiharakisha Isha. Akasema: 'Na mimi nadhani hivyo.'[89]

Hii ni dalili ya wazi kuwa tafsiri iliyotoka kwa Abu As-

88 *Naylul-Awtari*, Juz. 3, Uk. 217

89 *Musnad Ahmad*, Juz. 1, Uk. 221

Shauthau na wenzake, inatokana na wao kuzoea kutenganisha Sala na kuipa kila Sala wakati wake, hivyo wakadai kuipa kila Sala wakati wake ni faradhi isiyoachwa. Hivyo walipojikuta mbele ya riwaya hizi nyingi wakashindwa kujua makusudio ya riwaya, hivyo kila mmoja akakimbilia njia yake na Abu As-Shaathau akatafasiri kukusanya kwa kimuonekano.

**4. Alikusanya kwa sababu ya udhuru wa mvua**

Hii ndio tafsiri ya tatu ambayo amekimbilia kwayo yule asiyeruhusu kukusanya Sala mbili katika hali isiyo ya safari.

An-Nawawiy amesema: "Kati yao yupo aliyetafsiri kuwa kukusanya ni kwa ajili ya mvua. Kauli hii ndio mashuhuri toka kwa wanazuoni wakubwa waliotangulia."

Kisha akaijibu akasema: "Ni dhaifu kutokana na riwaya nyingine za pasipo na hofu wala mvua." [90]

Sababu kubwa ya kupatikana aina hii ya tafsiri ni kujaribu

[90] Sharhu ya *Sahih Muslim* ya An-Nawawiy, Juz, 5. Uk. 225

kulinganisha riwaya na fat'wa za wanazuoni wengi, kama si hivyo basi riwaya ziko wazi kuwa kukusanya ilikuwa bila udhuru wowote. Iwapo utafuatilia maelezo ya riwaya tulizonukuu toka kwa Ibnu Abbas utaishia kusema kuwa kukusanya haikuwa kwa udhuru fulani bali kwa ajili ya kuuondolea taabu umma wake.

Hivyo katika baadhi ya Hadithi utakuta kipengele: Pasipo na hofu wala safari (Angalia riwaya namba 1, 2, 15, 16, 18 na 23).

Katika nyingine. Pasipo na hofu wala mvua. (Angalia riwaya namba 3, 4, 11, 12, na 19).

Katika nyingine: Pasipo na safari wala mvua (Angalia riwaya ya 22). Katika nyingine: Pasi na hofu wala sababu. (Angalia riwaya ya 26).

Katika nyingine: Bila ugonjwa wala sababu (Angalia riwaya ya 28).

Zaidi ya hapo ni kuwa, **ila** iliyopokewa ndani ya riwaya ambayo ndio inapinga uwezekano huo iko wazi sana, na

yafuatayo ni maelezo yake: Katika baadhi ya riwaya **ila** ni kauli yake: Alitka asimsumbue yeyote kati ya watu wa umma wake (Angalia riwaya namba: 2, 3, 11, 12, na 23.) Katika baadhi ya riwaya nyingine: Ili umma wake usiwe na taabu. (Angalia riwaya ya 19).

Katika baadhi **ila** ni: Kuurahisisishia umma wake. (Angalia riwaya ya 22)

Katika baadhi ya riwaya nyingine: Asiutaabishe umma wake iwapo mtu akikusanya. (Angalia riwaya ya 25).

Katika baadhi ya riwaya nyingine: Ili umma wangu usi-taabike. (Angalia riwaya ya 30).

Hivyo mwenye kuzichunguza hizi riwaya anaamini kuwa kukusanya haikuwa kwa udhuru wa mvua wala safari, hofu wala **ila** nyingine, hivyo Mtume alikusanya Sala mbili Madina bila ya udhuru wowote, ikiwa ni amri toka kwa Mwenyezi Mungu ili aurahisishie umma wake, na ili asidhani mwenye kudhani kuwa kuipa kila Sala wakati wake ni faradhi ambayo hairuihusiwi kuikhalifu bali ni ubora usiyokatalika.

Hivyo kila mmoja ndani ya umma huu ana haki ya kukusanya bila kuipa kila Sala wakati wake.

**5. Alikusanya kwa sababu ya mawingu mbinguni**

Miongoni mwao yupo aliyetafsiri kuwa kulikuwa na mawingu hivyo akaswali Adhuhuri. Kisha mawingu yakaondoka na ikabainika kuwa wakati wa Al-Asr umeshaingia basi akaswali Al-Asr. Dhana hii ni dhaifu sana, hivyo aliyoyataja An-Nawawiy yanatosha kuonyesha udhaifu wake amesema: Japokuwa kuna mategemeo fulani ya dhana hii katika Adhuhuri na Al-Asr lakini hamna kabisa mategemeo ya dhana hii katika Magharibi na Isha. Tena kukusanya hakukuwa mahususi kwa ajili ya Adhuhuri na Al-Asr bali alikusanya Magharibi na Isha mpaka Ibnu Abbas akachelewesha Magharibi mpaka wakati wa Isha.[91]

Zaidi ya hapo ni kuwa laiti kukusanya kungekuwa ni kwa hali hiyo basi wapokezi wangeelezea wazi wazi. Hivi tunaweza kusema Ibnu Abbas alisahau sharti, au alikumbuka lakini hakulinukuu. Pia wenzake mfano wa Abu Huraira, Abdallah bin Omar na Abdallah bin Masudi.

91 Sharhu ya *Sahih Muslim*: Juz. 5, Uk. 225

## 6. Alikusanya kwa sababu ya ugonjwa

Baadhi ya wale wasiyopendezeshwa na kukusanya Sala mbili wametafsiri riwaya wakasema riwaya inamaanisha alikusanya kwa sababu ya udhuru wa ugonjwa au mfano wake.

Mtazamo huu kaunukuu An-Nawawiy toka kwa Ahmad bin Hambali,
Al-Qadhi Huseini mfuasi wa Shafi. Pia ameuchagua Al-Khatabiy, At-Tawaliy, na Al-Rawiyaniy wafuasi wa madhehebu ya Shafi.

An-Nawawiy ameuchagua akasema: Ndio mtazamo au chaguao katika tafsiri yake kutokana na dhahiri ya Hadithi na kitendo cha Ibnu Abbas` na uthibitisho wa Abu Huraira na kwa sababu ndani ya ugonjwa kuna taabu zaidi kuliko kwenye mvua. [92]

Anajibiwa kuwa: Tafsiri hii ni dhaifu na haifai kama tafsiri nyingine kwani ndani ya riwaya hizo kuna: Bila hofu wala ila. Na katika nyingine kuna: Bila ugonjwa wala ila. Na linalozidi kubatilisha hoja hiyo ni kuwa Ibnu

92 Sharhu ya *Sahih Muslim* ya An-Nawawiy Juz. 5, Uk. 226

Abbas alikusanya kati ya Magharibi na Isha huku akiwa si mgonjwa wala hakuna ugonjwa. Bali alikuwa akihutubia watu na maneno yake yakarefuka mpaka muda wa ubora wa Magharibi ukapita hivyo akaswali Magharibi na Isha ndani ya wakati mmoja.

Pia ni kuwa, laiti ingekuwa kuchelewesha ni kwa ajili ya ugonjwa basi ingesihi kwa mgonjwa mweyewe binafsi si kwa yule asiye mgonjwa, lakini Mtume alikusanya yeye na swahaba zake wote, hivyo kudhania kuwa wote walikuwa ni wagonjwa ni dhana iliyo mbali na ukweli. [93]

Kutokana na tuliyoyataja ndio maana Al-Hafidhu Ibnu Hajari Al-Asqalaniy amesema: "Laiti angekusanya kwa sababu ya ugonjwa basi asingeswali na yoyote isipokuwa na yule mwenye udhuru kama wake. Na dhahiri ni kuwa aliswali na maswahaba zake. Hilo kalitamka wazi Ibnu Abbas katika riwaya yake." [94]

Huyu hapa Al-Khatabiy anaelezea ndani ya (*Maalimu*) toka kwa Ibnul-Mundhir kuwa alisema: "Wala hakuna maana yoyote ya kulinasibisha jambo hili na udhuru

93 Angalia *Naylul-Awtari* ya As-Shaukaniy Juz. 3, Uk. 216

94 *Fathul-Baariy*, uk. 24

wowote kwa sababu Ibnu Abbas ameelezea ila yake akasema: "Alitaka asiutaabishe umma wake."

Na imeelezwa toka kwa Ibnu Sirin kuwa alikuwa haoni ubaya kukusanya Sala mbili kwa sababu ya haja fulani au kitu fulani iwapo tu hafanyi mazowea.[95]

Muhakiki wa *Sunanut-Tirmidhi* baada ya kunukuu maneno ya Al-Khatabiy amesema: Na hili ndio sahihi inayopatikana ndani ya Hadithi. Ama tafsiri ya ugonjwa au udhuru au jambo lingine ni kulazimisha jambo wala halina dalili. Kwa kuchukua sahihi hii watu wengi wame-ondolewa taabu kwani kazi zao na mazingira yao magu-mu yanaweza kuwalazimisha kukusanya Sala mbili hivyo wakajikuta wanapata dhambi au wanataabika katika hilo, hivyo katika kukusanya kuna raha kwao na msaada wa kumtii Mwenyezi Mungu iwapo tu hawatofanya kuwa ni mazoea kama alivyosema Ibnu Sirin. [96]

---

95 *Maalimus-Sunnani*, Juz. 1, Uk. 65

96 *Sunanut-Tirmidhiy*, Juz. 1, Uk. 358 Upande wa nyongeza kwa kalamu ya Ahmad Muhammad Shakir

Aliyoyasema ni haki lakini (Ibnu Sirin) kabana kile alichokipanua Mtume kwani kahusisha kukusanya kwa mwenye haja tu. Ilihali Mtume amepanua kwa watu wote kwa amri toka kwa Mwenyezi Mungu kwa yule mwenye ila au asiye na ila.

Ndio hakuna shaka kuwa kuipa kila Sala wakati wake wa ubora ni bora kuliko kuiswali ndani ya wakati wa kushirikiana, kwa hiyo kwa mujibu wa sheria ni kuwa muda wa kutekeleza Sala ni mpana.

## Alikusanya kwa sababu ya udhuru usiyojulikana

Kwa kuwa kuainisha udhuru unaoruhusu kukusanya imekuwa ni jambo gumu hivyo baadhi yao wamepita njia ya kutokujulikana na kutokuwa wazi, hivyo wakadai kuwa alikusanya kwa sababu ya udhuru unaoruhusu hilo lakini bila kuuainisha.

Kati ya watu waliounga mkono dhana hii ni Mufti wa zamani wa Saudia Abdul-Azizi bin Bazi katika ufafanuzi

wake mfupi wa Kitabu *Fat-hul-Bari fi sharhi Sahihl-Bukhari* Baada ya kudhoofIsha mtazamo wa Ibnu Hajar kuhusu maana ya kukusanya (kukusanya kimuonekano) kwa kusema: Kukusanya kwa namna hii ni dhaifu.

Akasema: Sahihi ni kuitafsiri Hadithi iliyotajwa kuwa alikusanya Sala zilizotajwa kwa sababu ya taabu iliyopatikana siku hiyo kutokana na ugonjwa uliozidi au baridi kali au matope na mfano wa hayo. Na dalili juu ya hilo ni kauli ya Ibnu Abbas alipoulizwa kuhusu ila ya kukusanya huku, akasema: "Ili asiutaabishe umma wake."

Kisha (Ibnu Bazi) akapendekeza kukusanya huku akasema: Nako ni jawabu kubwa sahihi lenye kutibu."**[97]**

Anajibiwa kuwa: Kukusanya huku na kule alikokudhoofisha kote ni dhaifu, kwa sababu kunapingana na riwaya na kitendo cha Ibnu Abbas, kwani yeye alikusanya Sala mbili huko Basra bila ya kuwa na ugonjwa mkali au baridi kali au matope.

---

[97] *Fathul-Bari fi Sharhu Sahihl- Bukhari*, Juz. 2, Uk. 24 maelezo ya Abdul-Azizi bin Bazi

Zaidi ya hapo ni kule kuenea kwa ila. Yaani kuuondolea taabu umma, kwani taabu haihusu hali za udhuru tu bali inajumuisha hata kuwalazimisha watu kutenganisha Sala kwa namna ya wajibu ndani ya maisha yao.

Hapa si vibaya kunukuu maneno ya Ibnu As-Siddiq yaliyomo ndani ya kitabu chake kiitwacho I*zalatul-Hadhari aman jamaa bayna salatayni fil-hadhar*, amesema: "Hakika Mtume (s.a.w.w.) elieleza wazi kuwa alifanya hivyo kwa lengo la kuuondolea umma wake taabu.

Akawabainishia kuwa inaruhusiwa iwapo wakihitajia kufanya. Hivyo kusema kuwa ila ni mvua baada ya kuwa tayari Mtume na maswahaba wapokezi wameshabainisha ila yake ni nini, itakuwa ni kuzuwa dhahiri isiyokuwepo bali itakuwa ni kuwapinga maswahaba na kumkosoa Mwenyezi Mungu na Mtume Wake.

Kwa sababu laiti angefanya hivyo kwa ajili ya mvua basi Mtume asingeeleza kinyume, wala wapokezi wasingeacha ila husika na kushikilia ila ya kuondoa taabu.

Pia imepokewa toka kwa Mtume kuwa katika usiku wenye mvua alikuwa akimwamrisha mtu anadi: "Salieni majumbani kwenu”. Wala hawakutaja hili katika kukusanya, ndio itakuwaje wataje ilihali wameshakanusha mvua?

Akaongeza kwa kusema: “Hakika Ibnu Abbas mpokezi wa Hadithi hii alichelewesha Sala akakusanya kwa ajili ya kujishughulisha na hotuba, kisha akatumia hoja ya kitendo cha Mtume kukusanya. Hairuhusiwi kutumia hoja ya kitendo cha Mtume kukusanya kwa ajili ya mvua kuthibitisha kitendo cha kukusanya kwa ajili ya hotuba au somo. Ilihali (Ibnu Abbas) alikuwa anaweza kusitisha kwa ajili ya Sala kisha baadae aendelee au amalize somo au hotuba uingiapo wakati wa Sala na wala asipate madhara yoyote wala taabu yoyote kama taabu na madhara yampatayo mtu atokapo wakati wa mvua na matope. [98]

**Matokeo**: Sheria hii toka kwa Mtume aliyopewa na Mwenyezi Mungu ni sheria ya raha inayoweza kutumika zama zote na katika hali zote za maisha ya kisasa vyovy-

98 *Izalatul-Hadhari aman jamaa bayna salatayni fil-hadhari*, 116-120

ote yatakavyokuwa.

Atakayechunguza kwa undani maisha ya kisasa ya ki-Magharibi ya biashara na viwanda ataona kuwa kutenganisha kati ya Sala mbili hasa Adhuhuri na Al-Asr ni jambo gumu na taabu kwa Waisilamu hasa wafanyakazi na watumishi. Kiasi kwamba inafikia ima akubali taabu au aache Sala, na inawezekana ikampelekea kukataa faradhi.

Wanazuoni wa sharia wa kisunni wenye mwamko wachukulie umuhimu ndani ya ijtihadi na hesabu zao msamaha huu uliyotolewa na Uislamu, na wepesi ulioletwa na riwaya. Wawatangazie watu waziwazi kuwa kukusanya Sala mbili Adhuhuri na Al-Asr, Magharibi na Isha ni jambo lililoruhusiwa kisheria japokuwa kutenganisha ni bora.

Hivyo atakaetenganisha atapata ubora wa kutenganisha na atakayekusanya atakuwa katekeleza faradhi ndani ya wakati wake.

## Maswali na Majibu

Kisha yule asiyeruhusu kukusanya Sala mbili amepinga kwa hoja mbali mbali huku akitumia Hadithi ya Ibnu Abbas na za wengine kama hoja katika suala hili. Zifuatazo ni hoja zake na majibu yake:

**Ya kwanza: Mgongano wa Hadithi ya kukusanya na ile ya hanashu:**

Habari za kukusanya zinapingana na habari aliyoitoa At-Tirmidhiy toka kwa Hanash toka kwa Ikrima toka kwa Ibnu Abbas toka kwa Mtume alisema kuwa: "Atakayekusanya kati ya Sala mbili bila udhuru wowote atakuwa kaja kwenye mlango kati ya milango ya madhambi makubwa." [99]

Nasema: kuwepo Hanash katika mapokezi yake ni dalili tosha juu ya udhaifu wa riwaya hii, na Hanashi ni lakabu

99 *Sunanut-Tirmidhiy*: Juz. 1, Uk. 356

ya Huseini bin Qaysi Ar-Rahbiy Al-Wasitwiy na yeye ni dhaifu mkubwa!

Ahmad amesema: “Huachwa.”

Bukhari amesema: “Hadithi zake hukanushwa wala haiandikwi Hadithi yake.”
Abu Zar'ati na Ibnu Mu'ini wamesema: “Ni dhaifu.” An-Nasaiy amesema: “Si mkweli.”

Marat amesema: “Huachwa.” As-Saadiy amesema: "Hadithi zake hukanushwa sana.” Ad-Daruqutniy amesema: “Huachwa.” Na Al-Dhahabiy ameiweka Hadithi hii katika fungu la Hadithi zinazokanushwa. [100]

Al-Uqayly amezungumzia Hadithi yake: “Atakayekusanya kati ya Sala mbili bila udhuru wowote atakuwa kaja kwenye mlango kati ya milango ya madhambi makubwa.” Akasema: “Haifuatwi wala haijulikani isipokuwa kupitia yeye, wala haina chanzo. Imesihi toka kwa Ibnu Abbas kuwa Mtume alikusanya kati ya Adhuhuri na Al-Asr.” [101]

100 *Mizanul-Itidali*, Juz. 1, Uk. 546 maelezo namba 2043

101 *Tahdhibut-Tahadhibu*, Juz. 1, Uk. 538

Ninaongeza kuwa katika mapokezi yake yumo Ikrima ambaye naye ni dhaifu, Hadithi zake haziwi hoja.

**Ya pili: Mgongano wa Hadithi ya kukusanya na ile ya usiku wa harusi**

Huenda mtu akadhani kuwa riwaya zinazoruhusu kukusanya Sala mbili kwa halisi zinapingana na Hadithi ya usiku wa harusi aliyoipokea Muslim.

Al-Alusiy ameinukuu ndani ya tafsiri yake toka kwa Ibnul-Hamam kwa kusema: "Ibnul-Hamam amesema: 'Hakika Hadithi ya Ibnu Abbas inapingana na aliyoyapokea Muslim katika Hadithi ya usiku wa harusi kuwa Mtume alisema: Usingizini hakuna uzembe bali uzembe ni katika hali isiyo ya usingizi kwa mtu kuchelewesha Sala mpaka uingie wakati wa Sala nyingine."

Al-Alusiy baada ya kunukuu maneno haya ya Ibnul-Hamam alisema: Kuna nukta nyingi za kuhoji.[102]

102 *Ruhunil-Maani*, Juz. 15 Uk. 134 tafsiri ya Aya: "Simamisha Sala lipindukapo jua"

Katika mdahalo huu kuna nukta nyingi za kuhoji bali za kujibu.

**Kwanza**: Hadithi ya harusi haijumuishi kukusanya kwa kutanguliza bali inahusika na kukusanya kwa kuchelewesha tu kwani alisema: "Kuchelelewesha Sala mpaka uingie wakati wa Sala nyingine."

**Pili**: Kitendo cha Ibnu Abbas kinaonyesha kuwa kukusanya kwa Mtume kulikuwa kwa kuchelewesha kwa mujibu wa riwaya aliyopokea Muslim kama ilivyotangulia kuwa: Siku moja Ibnu Abbas alitutolea muhadhara baada ya Al-Asr mpaka lilipokuchwa jua na nyota zikaanza kuonekana. Watu wakawa wanasema: 'Sala! Sala! Mara akaja mtu mmoja wa koo ya Bani Tamim huku akisisitiza: Sala! Sala! Ndipo aliposema Ibnu Abbas: 'Je unanifundisha Sunna? Eee usiye na mama we!' Kisha akasema: 'Nilimuona Mtume amekusanya baina ya Adhuhuri na Al-Asr, na Magharibi na Isha.' Abdallah bin Shaqiqi anasema: 'Hilo likanitia shaka moyoni mwangu, mara moja nikaenda kwa Abu Huraira nikamuuliza, akathibitisha habari ya Ibnu Abbas kuwa ni kweli."[103]

---

103 Angalia riwaya namba 6

Ni Hadithi ipi kati ya hizo mbili inafaa kuchukuliwa? Hadithi inamaanisha kuchelewesha Sala ya Isha mpaka unaingia wakati wa Sala ya alfajiri, linalounga mkono maana hii ni kupatikana riwaya katika usiku wa harusi, usiku ambao mtu anajishughulisha na mambo mpaka wakati wa alfajiri unaingia.

**Ya tatu: Hadithi ya Habib bin Thabiti si hoja**

Riwaya ya tatu aliyoitoa Muslim ndani ya upokezi wake yumo Habib bin Abi Thabiti.

Al-Khatabi ndani ya *Maalimu* yake ameizungumzia akasema: "Hadithi hii hawaisemi wanazuoni wengi zaidi wa sheria, upokezi wake ni safi isipokuwa hawakuzungumza kuhusu Habib." [104]

Anajibiwa kuwa: Kusema kuwa wanazuoni wengi wa sheria hawaisemi ni kweli, lakini wapo wanaoisema na kuitolea fat'wa, majina yao yameshatangulia. Ama kuhusu wanazuoni wengi sababu ya kutokuichukua ima ni kwa kuwa kutenganisha ndio kunakubaliana na ubora

104 *Maalimus-Sunan*, Juz. 2, Uk. 55, Hadith Na. 1167

(Ihtiyati), au kwa kuwa inatofautiana na hali aliyoendelea nayo Mtume.

Ama kuhusu ubora ni kuwa imeshatangulia kuwa katika mazingira yetu haya kutoa fat'wa ya kutenganisha ni kinyume na ubora, kwa sababu fat'wa hiyo inapelekea watu kuacha Sala.

Ama kuhusu kitendo cha Mtume ni kuwa yeye mwenyewe alikusanya ili aufahamishe umma wake kuwa kuendelea kwake kutenganisha ni Sunna wala si faradhi.

Ama aliyoyasema kuhusu dosari walizozungumza juu ya Habib bin Thabit ni kinyume na aliyoyataja Ad-Dhahabiy ndani ya kitabu *Mizanul-iitidal* kwani amesema: "Watu wote wa *Sahih Sita* wametoa hoja kutumia Hadithi hii bila kusita. Akasema: Yahya bin Mu'ini: na jamaa wamethibitisha ukweli wake." **[105]**

Zaidi ya hapo ni kuwa riwaya hii inapatikana ndani ya moja kati ya *Sahih* mbili ambazo masunni wameafikiana juu ya usahihi wa Hadithi zake na juu ya kufanyia kazi yaliyomo humo.

105 *Mizanul-Itidal*, Juz. 10, Uk. 1690

Na mwisho wa dua yetu ni kumshukuru Mwenyezi Mungu Bwana wa ulimwengu wote.

**Imetarjumiwa na:**
**Hemedi Lubumba Selemani**
**0773- 017178**
**0715- 017178**
**0754- 017178**
**Dar es Salaam.**

ORODHA YA VITABU VILIVYO CHAPISHWA NA
AL-ITRAH FOUNDATION

1. i) Qur'ani Tukufu – Pamoja na Tarjuma ya Kiswahili
   ii) Qur'an Al-Kariim - Tafsir Al-Kashif Juzuu ya kwanza mpaka Thelathini
2. Uharamisho wa Riba
3. Uharamisho wa uwongo Juzuu ya Kwanza
4. Uharamisho wa uwongo Juzuu ya Pili
5. Hekaya za Bahlul
6. Muhanga wa Imamu Husein (A.S.)
7. Mikingamo iliyomzunguka Imamu Ali (A.S.)
8. Hijab vazi Bora
9. Ukweli wa Shia Ithnaashari
10. Madhambi Makuu
11. Mbingu imenikirimu
12. Abdallah Ibn Saba
13. Khadijatul Kubra
14. Utumwa
15. Umakini katika Swala
16. Misingi ya Maarifa

17. Kanuni za Ndoa na maadili ya Familia
18. Bilal wa Afrika
19. Abudhar
20. Usahihi wa Historia ya Uislamu na Waislamu
21. Salman Farsi
22. Ammar Yasir
23. Qur'an na Hadithi
24. Elimu ya Nafsi
25. Yajue Madhehebu ya Shia
26. Ukusanyaji na Uhifadhi wa Qur'an Tukufu
27. Al-Wahda
28. Ponyo kutoka katika Qur'an
29. Uislamu mfumo kamili wa maisha ya kijamii
30. Mashukio ya Akhera
31. Al Amali
32. Dua kwa Mujibu wa Ahlulbayt (a.s)
33. Udhuu kwa Mtazamo wa Qur'ani na Sunna
34. Haki za wanawake katika Uislamu
35. Mwenyezi Mungu na sifa zake
36. Kumswalia Mtume (s)
37. Nafasi za Ahlul Bayt (a.s)
38. Adhana

39. Upendo katika Ukristo na Uislamu
40. Qur'ani na Kuhifadhiwa Kwake
41. Maana ya laana na kutukana katika Qur'ani Tukufu
42. Kupaka juu ya khofu
43. Kukusanya Sala Mbili
44. Bismillah ni sehemu ya Qur'ani na husomwa kwa Jahara
45. Kuwaongoza vijana wa kizazi kipya
46. Kusujudu juu ya udongo
47. Kusheherekea Maulidi Ya Mtume (s)
48. Tarawehe
49. Malumbano baina ya Sunni na Shia
50. Kupunguza Swala safarini
51. Kufungua safarini
52. Umaasumu wa Manabii
53. Qur'an Yatoa Changamoto
54. as-Salaatu Khayrun Mina -'n Nawm
55. Uadilifu wa Masahaba
56. Dua e Kumayl
57. Sauti Ya Uadilifu wa Binadamu
58. Umaasumu wa Mitume - Faida Zake Na Lengo Lake
59. Umaasumu wa Mitume - Majibu Ya Aya Zenye Utata
60. Umaasumu wa Mitume - Umaasumu wa Mtume Muhammad (s)

61. Nahju'l-Balaghah - Juzuu ya Kwanza
62. Nahju'l-Balaghah - Juzuu ya Pili
63. Kuzuru Makaburi
64. Maswali Na Mishkili Elfu - Sehemu ya Kwanza
65. Maswali Na Mishkili Elfu - Sehemu ya Pili
66. Maswali Na Mishkili Elfu - Sehemu ya Tatu
67. Maswali Na Mishkili Elfu - Sehemu ya Nne
68. Maswali Na Mishkili Elfu - Sehemu ya Tano
69. Maswali Na Mishkili Elfu - Sehemu ya Sita
70. Tujifunze Misingi Ya Dini
71. Sala ni Nguzo ya Dini
72. Mikesha Ya Peshawar
73. Malezi Ya Mtoto Katika Uislamu
74. Ubora wa Imam 'Ali na Ushia ndio njia iliyonyooka
75. Hukumu za Kifikihi zinazowahusu Wanawake
76. Liqaa-u-llaah
77. Muhammad (s) Mtume wa Allah
78. Amani na Jihadi Katika Uislamu
79. Uislamu Ulienea Vipi?
80. Uadilifu, Amani na Mtume Muhammad (s)
81. Dhana ya Ndoa ya Mitala na Ndoa za Mtume Muhammad (s)
82. Urejeo (al-Raj'ah)

83. Mazingira
84. Utokezo (al - Badau)
85. Hukumu ya kujenga juu ya makaburi
86. Swala ya maiti na kumlilia maiti
87. Uislamu na Uwingi wa Dini
88. Mtoto mwema
89. Adabu za Sokoni Na Njiani
90. Johari za hekima kwa vijana
91. Maalimul Madrasatain Sehemu ya Kwanza
92. Maalimul Madrasatain Sehemu ya Pili
93. Maalimul Madrasatain Sehemu ya Tatu
94. Tawasali (AT- TAWASSUL)
95. Imam Mahdi katika Usunni na Ushia
96. Hukumu za Mgonjwa
97. Sadaka yenye kuendelea
98. Msahafu wa Imam Ali
99. Maimamu wa Ahlul Bait – Ujumbe na Jihadi
100. Idi Al-Ghadir
101. Kusoma sura zenye Sijda ya wajibu
102. Hukumu zinazomuhusu mkuu wa kazi na Mfanyakazi
103. Huduma ya Afya katika Uislamu
104. Sunna za Nabii Muhammad (saww)

105. Historia na sera ya viongozi wema (Sehemu ya Kwanza)
106. Historia na sera ya viongozi wema (Sehemu ya Pili)
107. Shahiid Mfiadini
108. Mwanamke Na Sharia
109. Ujumbe -Sehemu ya Kwanza
110. Ujumbe - Sehemu ya Pili
111. Ujumbe - Sehemu ya Tatu
112. Ujumbe - Sehemu ya Nne
113. Mariamu, Yesu na Ukristo kwa mtazamo wa Kiislamu
114. Hadithi ya Thaqalain
115. Ndoa ya Mutaa
116. Ukweli uliopotea sehemu ya Kwanza
117. Ukweli uliopotea sehemu ya Pili
118. Ukweli uliopotea sehemu ya Tatu
119. Ukweli uliopotea sehemu ya Nne
120. Ukweli uliopotea sehemu ya Tano
121. Mkutano wa Maulamaa wa Baghdad
122. Safari ya kuifuata Nuru
123. Fatima al-Zahra
124. Myahudi wa Kimataifa
125. Kuanzia ndoa hadi kuwa Wazazi
126. Visa vya kweli sehemu ya Kwanza

127. Visa vya kweli sehemu ya Pili
128. Elimu ya Ghaibu ya Maimamu
129. Mwanadamu na Mustakabali wake
130. Imam Ali ('a) Ndugu wa Mtume Muhammad (s)
 (Sehemu ya Kwanza)
131. Imam Ali ('a) Ndugu wa Mtume Muhammad (s)
 (Sehemu ya Pili)
132. Khairul l'Bariyyah
133. Uislamu na mafunzo ya kimalezi
134. Vijana ni Hazina ya Uislamu
135. Adhana ni Ndoto au ni Wahyi?
136. Tabaruku
137. Saada Kamili – Kitabu cha Kiada cha Maadili
138. Vikao vya furaha
139. Shia asema haya Sunni asema haya Wewe wasemaje?
140. Visa vya wachamungu
141. Falsafa ya Dini
142. Kuhuzunika na Kuomboleza
143. Sunna katika Kitabu Fiqhi al-Sunnah
144. Mjadala wa Kiitikadi
145. Kuonekana kwa Allah
146. Tabia njema kwa Mujibu wa Ahlul-Bayt (Sehemu ya Kwanza)

147. Tabia njema kwa Mujibu wa Ahlul-Bayt (Sehemu ya Pili)
148. Ndugu na Jirani
149. Ushia ndani ya Usunni
150. Maswali na Majibu
151. Mafunzo ya hukmu za ibada
152. Ahlul Bayt ndani ya tafsiri za Kisunni No 1
153. Ahlul Bayt ndani ya tafsiri za Kisunni No 2
154. Ahlul Bayt ndani ya tafsiri za Kisunni No 3
155. Abu Huraira
156. Vipengee kadhaa katika Swala ya Jamaa na Msikiti.
157. Mazingatio kutoka katika Qur'an - Sehemu ya Kwanza
158. Mazingatio kutoka kaitka Qur'an - Sehemu ya Pili
159. Mazingatio kutoka katika Uislamu - Sehemu ya kwanza
160. Mazingatio kutoka katika Uislamu - Sehemu ya Pili
161. Shia na Qur'ani – Majibu na Maelezo
162. Falsafa ya Mageuzi ya Imam Husein (a.s)
163. Amali za Mwezi Mtukufu wa Ramadhani
164. Elimu ya Tiba za Kiislamu - Matibabu ya Maimamu
165. Uislamu Safi
166. Majlisi za Imam Husein Majumbani
167. Je, Kufunga Mikono
168. Uislam wa Shia

169. Amali za Makka
170. Amali za Madina
171. Asili ya Madhehebu katika Uislamu
172. Sira ya Imam Ali kuhusu Waasi
173. Ukweli uliofichika katika neno la Allah
174. Uislamu na Mifumo ya Uchumi
175. Umoja wa Kiislamu na Furaha
176. Mas'ala ya Kifiqhi
177. Jifunze kusoma Qur'ani
178. as-Sahifatul Kamilah as-Sajjadiyyah
179. Hayya 'Alaa Khayri'l-'Amal Katika Adhana
180. Ukweli kuhusu Funga ya Siku ya Ashura
181. Dua za Miezi Mitatu Mitukufu (Rajabu, Shaabani na Ramadhani)
182. Uadilifu katika Uislamu
183. Mahdi katika Sunna
184. Maswali Ya Uchunguzi Kuhusu Uislam
185. Kazi na Bidii ni njia ya maendeleo
186. Abu Talib – Jabali Imara la Imani
187. Ujenzi na Utakaso wa Nafsi
188. Vijana na Matarajio ya Baadaye
189. Historia maana na lengo la Usalafi

190. Ushia – Hoja na Majibu
191. Mateso ya Dhuria wa Mtume (saww)
192. Maombolezo – Msiba wa Bwana wa Mashahidi (a.s.)
193. Shahidi kwa Ajili ya Ubinadamu
194. Takwa
195. Upotoshaji Dhahiri katika (Turathi) Hazina ya Kiislamu
196. Amirul Muuminina ('as) na Makhalifa
197. Tawheed Na Shirki
198. Kuvunja hoja iliyotumika kutetea Uimamu wa AbuBakr
199. Adabu za vikao na mazungumzo
200. Hija ya Kuaga
201. Uwazi baina ya Maslahi na Vikwazo
202. Fadhila za watukufu watano katika Sahih Sita
203. Mdahalo baina ya Mwanachuoni wa Kisunni na Kishia (Al- Muraja'aat)
204. Utawala na Uendeshaji katika Sera ya Imam Ali (as)
205. Imam Husain ni Mfumo wa Marekebisho na Mageuzi
206. Mtazamo kuhusu msuguano wa Kimadhehebu
207. Nchi na Uraia – Haki na wajibu kwa Taifa
208. Mtazamo wa Ibn Taymiyyah juu ya Imam Ali (as)
209. Uongozi wa Kidini – Maelekezo na Utekelezaji wa Kijamii
210. Maadili ya Ashura

211. Mshumaa – Shahidi na Kifo cha Kishahidi
212. Mizani ya Hekima – Hadithi za Ahlul Bait (as) – Sehemu ya Kwanza
213. Imam Ali na Mambo ya Umma
214. Imam Ali na Mfumo wa Usawa
215. Uimamu na Tamko la Kutawazwa
216. Mfumo wa Wilaya
217. Vipi Tutaishinda Hofu?
218. Kumswalia Mtume ni Ufunguo wa Utatuzi wa Matatizo
219. Maeneo ya Umma na Mali Zake
220. Nahju 'L-Balagha – Majmua ya Khutba, Amri, Barua, Risala, Mawaidha na Semi za Amirul-Muuminin Ali bin Abu Talib (a.s.)
221. Mukhtar – Shujaa aliyelipiza kisasi dhidi ya wauaji wa Imam Husein (as) hapo Karbala
222. Mazingatio Katika Swala
223. Imam Hasan na Mfumo wa Kujenga Jamii
224. Vyakula Na Vinywaji
225. Kuelewa Rehema ya Mwenyezi Mungu
226. Tiba ya Maradhi ya Kimaadili
227. Yafaayo kijamii
228. Shia Na Hadith - Majibu na Maelezo

229. Mkakati wa Kupambanana Ufakiri
230. Mtazamo Mpya - Mwanamke katika Uislamu
231. Taqiyya Kwa Mujibu Wa Sheria Ya Kiislamu
232. Imam Mahdi Na Bishara Ya Matumaini
233. Jihadi
234. Majanga Na Jukumu La Jamii
235. Muhadhara wa Maulamaa
236. Mashairi ya Kijamii
237. Ngano ya kwamba Qur'ani imebadilishwa
238. Mwanamke Katika Harakati Za Mageuzi
239. Shia Na Sahaba - Majibu na Maelezo
240. Yusuf Mkweli
241. Hotuba Za Kiislamu Juu ya Haki Za Binadamu
242. Ugaidi wa Kifikra katika Medani ya Kidini

KOPI NNE ZIFUATAZO ZIMETAFSIRIWA
KWA LUGHA KINYARWANDA

1. Amateka Ya Muhammadi (s.a.w.w) Na Aba' Khalifa
2. Nyuma yaho naje kuyoboka
3. Amavu n'amavuko by'ubushiya
4. Shiya na Hadithi

OORODHA YA VITABU VILIVYO CHAPISHWA NA
AL-ITRAH FOUNDATION KWA LUGHA YA KIFARANSA

1. Livre Islamique

BACK COVER

KUKUSANYA SALA MBILI

Sheria ya Kiislamu ni ya kipekee kwa kuwa inahusika na kila jambo huku ikiweka utatuzi wa matatizo yote yanayompata mwanadamu katika sekta zote za maisha yake, hivyo Mwenyezi Mungu akasema:

"Leo nimewakamilishieni dini yenu na kuwatimizieni neema Yangu na nimewapendeleeni Uislamu uwe dini yenu." (5:3).

Isipokuwa kuna masuala madogo madogo ambayo wanazuoni wa sheria wamehitilafiana kwa sababu ya kutofautiana kwao kuhusu riwaya ambazo zimenasibishwa kwa Mtume. Jambo ambalo limesababisha kutofautiana kuhusu masuala madodo madogo ya sheria.

Kwa kuwa ukweli hutokana na utafiti basi hakika katika mtiririko wa masomo haya mwandishi amejaribu kuliweka sala hili juu ya

meza ya utafiti, kwani huenda ikawa ndio njia ya kuunganisha mtazamo na kusogeza hatua katika uwanja huu. Kwani tofauti iliyopo si katika asili na misingi ya dini hata isababishe kuwa na uadui na chuki, bali tofauti iliyopo ni kuhusu riwaya zilizonasibishwa na Mtume, nalo ni jambo dogo ukilinganisha na mambo mengi ambayo tunaafikiana kati ya madhehebu za Kiislamu. Na mwongozo wetu katika njia hii ni kauli ya Mwenyezi Mungu:

"Na shikamaneni katika kamba ya Mwenyezi Mungu nyote wala msifarakiane. Na kumbukeni neema ya Mwenyezi Mungu iliyo juu yenu, mlipokuwa maadui na akaziunganisha nyoyo zenu, hivyo kwa neema Zake mkawa ndugu." (3:103)

Kimetolewa na kuchapishwa na:
Al-Itrah Foundation
P.O. Box 19701,
Dar es Salaam, Tanzania
Simu: +255 22 2110640
Fax: +255 22 2131036
Email: info@alitrah.org